# Nipashe

Jumamosi Juni 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580980

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebo... ashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,006,442,235/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Talaka** zatajwa kuwa maficho ya ukatili wa kijinsia nchini

UKURASA 4




**POGBA AKUBALI KUSAINI MIAKA MINNE JUVE**

UKURASA 21



MBUNGE AFICHUA:

# Hivi ndivyo ulivyo ulaji wa mabilioni katika halmashauri

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MAHAKAMA YAWAACHIA HURU WAFANYAKAZI NEMC**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru wafanyakazi wawili wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa...

UKURASA WA 5

**WAANDAMANA UBALOZI KENYA MADAI UPOTOSHAJI**

KUNDI la Jamii ya Wamaasai kutoka maeneo mbalimbali nchini limeandamana kuelekea Ubalozi wa Kenya nchini...

UKURASA WA 7

**BIL. 60/- ZAKUSANYWA TOZO DARAJA LA NYERERE**

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu, Mfuko wa NSSF umekusanya...


## Mkurugenzi Jiji Arusha kortini kwa kesi mbili za uhujumu

UKURASA 2




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana (kulia), akikabidhi hati ya umiliki ardhi ya makazi kwa mzee wa kimila wa Kimasai, Laigwanani Matingoi, katika Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga jana, ambako zimehamia familia 20 zilizotoka kwa hiyari Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



## Zumaridi adai kutishiwa kuuawa akiwa gerezani

UK. 2


**MICHEZO** **MPOLE AZITEGA SIMBA, YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Hivi ndivyo mabilioni yanaliwa halmashauri

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, ameitaka serikali kuzibana halmashauri ambazo zina matumizi makubwa kiasi cha kufikia hatua viongozi wake kugawana fedha kwenye akaunti zao binafsi na kununua magari.

Akichangia mjadala wa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha bungeni jana, Gambo alisema ni lazima serikali inapobana matumizi, kuangalia fedha za matumizi kwa baadhi ya halmashauri ambazo zinaonekana kutapanya.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lina makadirio ya Sh. bilioni 81 zikijumuisha mapato ambayo aliyaita yasiyolindwa Sh. bilioni 62.2 ikitolewa asilimia 70 ya maendeleo ambayo ni Sh. 43.587, Sh. bilioni 18 ni kwa ajili ya matumizi mengine kama posho na mafuta.

Gambo alisema kwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma makisio ya mapato ni Sh. bilioni 55, mapato yasiyolindwa ni Sh. bilioni 44, inayokwenda kwenye maendeleo asilimia 60 ni Sh. bilioni 26 huku matumizi ya kawaida Sh. bilioni 17.

Alisema Halmashauri ya Kinondoni makisio yake ni Sh. bilioni 57 na mapato yasiyolindwa ni Sh. bilioni 46, matumizi ya maendeleo ni Sh. bilioni 32 na hivyo kuwa na matumizi ya kawaida Sh. bilioni 14.

Mbunge huyo alisema Halmashauri ya Arusha makisio yake ni Sh. bilioni 30, mapato yasiyolindwa Sh. bilioni 24, asilimia 70 ya maendeleo ni Sh. bilioni 17 na matumizi ya kawaida ni Sh. bilioni saba.

"Tumeona mfano mmoja Jiji la Arusha kwa mapato ya Sh. bilioni saba wameingiziana fedha kwenye akaunti zao binafsi.

"Ushari wangu tunaomba Wizara ya Fedha na Mipango wakae na TAMISEMI badala ya kusema waangalie asilimia, waangalie matumizi halisi," alisema.

Kwa mujibu wa Gambo, matumizi ya Halmashauri ya Dar es Salaam pekee ni sawa na ya halmashauri ndogo 14 ambazo matumizi ya kawaida kwa mwaka ni Sh. bilioni 9.9. "Mimi nadhani kuna haja ya serikali kuangalia matumizi kwenye halmashauri, Rais anatafuta hela dunia nzima, anabana matumizi lakini Waziri wa Fedha na TAMISEMI msaidieni Arusha," alisema.

Alisema kwa Jiji la Arusha wanavyokula fedha, wakipewa Sh. bilioni tatu au nne zinawatosha na inayobakia ikajenge barabara, vituo vya afya na kupeleka huduma kwa wananchi.

Mbunge wa Kibamba, Issa Mtemvu, alitaka kuwe na viwango tofauti vya posho kwa madiwani kulingana na uwezo wa halmashauri kwa kuwa uwezo unatofautiana kutoka halmashauri moja hadi nyingine kukusanya fedha.

**MIAMALA YA SIMU**

Mbunge wa Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chaya, alitaka serikali kuwasilisha bungeni tathimini ya kodi ya miamala ya simu na ukusanyaji wa kodi ya majengo kupitia Luku.

"Sijasikia katika taarifa yako ukisema kwa kiwango gani tumefanikiwa kwenye vyanzo hivi, kwamba tunaweza kuendelea na miamala au kodi ya majengo kupitia luku,"alisema.

Kuhusu namba ya mlipa kodi, alisema ni wazo jema lakini serikali inapaswa kuondoa utitiri wa vitambulisho na kuwa kama nchi zingine ambazo mtoto anapozaliwa anapewa namba.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza na Viongozi wa Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, katika ukumbi wa Msekwa, Bungeni jijini Dodoma jana, wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Shekhe Alhad Mussa Salum (kulia kwake). **PICHA: BUNGE**

## Mkurugenzi Jiji Arusha kortini

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. John Pima, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, akikabiliwa na kesi mbili za uhujumu uchumi.

Dk. Pima na wenzake walipandishwa kizimbani jana majira ya saa nane mchana na kusomewa mashtaka manane katika kesi mbili zinazowakabili mahakamani huko.

Mbali na Dk. Pima, washtakiwa wengine ni: Innocent Maduhu, aliyekuwa Mchumi wa Jiji); Nuru Ginana (mchumi); Alex Daniel (mchumi); na Mariam Mshana (aliyekuwa Mweka hazina wa Jiji la Arusha na walisomewa mashtaka hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Bittony Mwakisu.

Hata hivyo, Mariam hakuwapo mahakamani huko na upande wa Jamhuri uliiomba mahakama kutoa hati ya wito wa kukamatwa kwa mshtakiwa huyo ambaye ni wa pili katika kesi zote.

Katika shauri hilo, Jamhuri iliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Akisa Mhando na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Hamidu Simbano.

Dk. Pima na Maduhu wanawakilishwa na Wakili Valentine Nyalu. Shauri la kwanza linawakabili Dk. Pima, Mariam, Maduhu na Ginana wanaokabiliwa na mashtaka manne ya ufujaji, ubadhirifu na matumizi ya nyaraka kwa lengo la kumdanganya mwajiri.

Washtakiwa hao wataendelea kuwa rumande kwa kuwa walishindwa kukidhi masharti ya dhamana.

Washtakiwa hao, kila mmoja alipaswa kuwa na wadhamini wawili watakaoweka bondi ya Sh. milioni 32 kama dhamana au kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Mwendesha Mashtaka Mwandamizi wa Serikali, Kissa Mhando akisoma mashtaka manne katika kesi namba 3/2022 mbele ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Arusha, Bitone Mwakisu, alidai watuhumiwa hao kwa pamoja, wakiwa waajiriwa wa TAMISEMI kati ya Aprill 14 mwaka huu na Aprill 16 mwaka huu, wakiwa na nia ovu, walifanya ubadhirifu wa Sh. milioni 67 kwa matumizi yao binafsi wakati wakijua wazi kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Katika kesi ya uhujumu uchumi namba 4/2022 iliyokuwa ikiwakabili Pima, Mshana (hakuwapo mahakamani), Maduhu na Alex Tihema (39), inadaiwa Aprill 14 mwaka huu na Aprill 16 mwaka huu, wote wanatuhumiwa kumdanganya mwajiri na kuchukua kiasi cha Sh. milioni 65 kwa matumizi yao binafsi wakati wakijua wazi kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Waendesha Mashtaka wa Serikali, Mhando na Simbano walidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na dhamana iko wazi iwapo watuhumiwa watazingatia masharti lakini watuhumiwa walishindwa masharti na kwenda gerezani hadi Julai Mosi mwaka huu, kesi yao itakapotajwa tena.

# Zumaridi adai kutishiwa kuuawa gerezani

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KESI ya Mchungaji Diana Bundala, maarufu Mfalme Zumaridi, imeingia katika sura mpya baada ya wakili wake kudai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza kwamba mteja wake anatishiwa kuawa katika Gereza la Butimba mkoani Mwanza.

Akihitimisha mahojiano na shahidi katika kesi hiyo namba 12 ya mwaka 2022 inayomkabili mchungaji huyo na wenzake 84 jana, Wakili wa Utetezi, Steven Kitale, alidai mteja wake akiwa gerezani amekuwa akitishiwa kuuawa na askari magereza huku wakipanga njama za kumtenga katika chumba cha pekee mahabusu huyo.

Wakili Kitale alidai askari magereza aliowataja kutoka Gereza la Butimba ambako mteja wake yuko, mahabusu wamemweleza Zumaridi kuwa hana muda mrefu katika gereza hilo atafanyiwa kitu chochote ili kuhakikisha anapoteza uhai wake.

Alidai askari hao wamekuwa wakimpatia mateso mbalimbali ambayo ni kinyume cha sheria kwa mtu ambaye bado ni mahabusu ikiwamo adhabu ya kutengwa na wenzake.

Wakili Kitale alidai kuwa huko mahabusu askari hao wamepanga kumhamisha chumba cha pamoja na kumtenga katika chumba chake na alitakiwa kuhamishwa Juni 16, yaani juzi lakini kwa kuwa shauri lake lilikuwa linaendelea mahakamani, walisitisha kufanya hivyo ili kusubiri atoke mahakamani.

Aliendelea kudai kuwa mteja wake amekuwa akinyimwa haki ikiwamo haki ya kuabudu kama ilivyo kwa waamini wengine wanaopatiwa haki na uhuru wa kuabudu.

Katika kesi hiyo jana, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Ruperto Mapunda ambaye ni Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Nyamagana, aliwasilisha ushahidi wake.

Alidai washtakiwa hao 84 pamoja na Mfalme Zumaridi, walikusanyika katika Ngome ya Mfalme Zumaridi isivyo halili kwa lengo la kutia hofu watu wa eneo hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Shahidi huyo alidai kuwa msafara uliokuwa na askari 43 pamoja mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa mtaa, waliwakamata watu 149 ambapo baada ya upelelezi, watu 84 pamoja na Mfalme Zumaridi ndio ambao walikutwa na tuhuma na kufunguliwa mashtaka.

Hakimu Mkazi Mwandamizi wa mahakama hiyo, Monica Ndyekobora, aliahirisha shauri hilo hadi Juni 30, 2022, kesi hiyo itakapoendelea kusikilizwa huku akiwataka mawakili wa utetezi kupeleka malalamiko yao kwa Mkuu wa Magereza kwa kuwa yapo nje ya uwezo wa mahakama.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, alipokuwa akitoa uchambuzi wa kituo hicho, kuhusu makadirio ya mapendekezo ya bajeti ya taifa ya mwaka 2022/2023 kwa mtazamo wa haki za binadamu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TANESCO yawasha mtambo mpya wa kuzalisha MW 45

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limewasha rasmi mtambo mmoja mpya wenye uwezo wa kuzalisha megawati 45 ambao unatarajiwa kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuzalisha nishati ya umeme nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Meneja wa mradi wa upanuzi wa Kituo cha Kinyerezi I, Abdallah Chikoyo, alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa mitambo minne ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia na kila mmoja una uwezo wa kuzalisha megawati 45.

Alisema mtambo huo uliowashwa ni miongoni mwa mitambo hiyo minne mipya inayosimikwa katika kituo hicho kwa ajili ya kutatua au kupunguza tatizo la kupungua au kukatika kwa umeme nchini.

"Mitambo hii ina uwezo wa kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 35 na itatusaidia kutuvusha wakati wa majanga ya ukame na itaimarisha uwezo wetu wa kuzalisha umeme kwenye Gridi ya Taifa.

"Pia una faida kwa sababu unatumia gesi asilia inayotoka ndani ya nchi na hakuna kununua mafuta kutoka nje kama ilivyokuwa awali," alisema Chikoyo.

Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Maharage Chande, alibainisha kuwa kipindi cha ukame kinachokuja, watakuwa vizuri na hawatakuwa na matatizo makubwa kama mwaka jana kutokana na kuongezeka kwa kasi ya uzalishaji wa umeme baada ya kukamilika kwa ujenzi wa mitambo hiyo.

"Nadhani ndo kitakuwa kipindi cha mwisho cha ukame ambacho kunakuwa na matatizo kwa sababu sasa hivi tunakuwa na mpango wa muda mrefu zaidi ili kuhakikisha wateja wetu Watanzania kinapofika kipindi kile, hali inakuwa nzuri," alisema Chande.

Aliongeza kuwa utaratibu uliopo kwa wasimamizi wa mradi huo kila baada ya wiki moja watakuwa wanawasha mtambo mmoja, huku akiahidi kuwa hadi ifikapo mwezi Desemba mwaka huu, yote itakuwa imeshafika kwenye Gridi ya Taifa.

Aliahidi kuwa kwa kuwashwa mitambo hiyo, Watanzania watarajie uwezo wa shirika hilo kukabiliana na ukame pale unapotokea, utaongezeka kwa kuwa itapeleka MW 185 kwenye Gridi ya Taifa.

"Watanzania watarajie uwezo na safari yete ya kuwa na umeme wa nafuu na uhakika tunaenda nayo, ila safari ni hatua huwezi kuruka moja kwa moja ukafika mwisho, unakwenda na hatua.

"Na hii ni mojawapo ambayo ni muhimu na mitambo mingine inaingia hivyo hadi 2024, tatizo la umeme halitakuwa katika kiwango kikubwa," alisema Chande.

# Mbunge apata ukakasi kodi majengo kwa Luku

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Ukonga (CCM), Jerry Silaa, amesema siyo sawa kwa mwenye nyumba wa Masaki jijini Dar es Saalam kutozwa kodi ya majengo ya Sh. 1,000 kwa mwezi na 12,000 kwa mwaka sawa na wa maeneo mengine.

Akichangia bungeni jana mjadala wa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, mbunge huyo alisema ni wakati wa tozo hiyo kurudi halmashauri ili ikusanywe kwa ufanisi kama awali.

"Kodi ya majengo ilichukuliwa ikapelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), lakini ripoti haikuwahi kuletwa hapa kujua ukusanyaji wake, na haikukusanywa kwa ufanisi kama zilivyokuwa zinakusanya, mwaka jana mkachukua mkapeleka kwenye nyumba, nyumba ya Masaki inalipa Sh. 1,000 kwa mwezi, Sh. 12,000 kwa mwaka.

"Ikirudishwa kwenye halmashauri utengenezwe utaratibu asilimia tano ibaki kwenye mtaa, asilimia tano ibaki kwenye kata isaidie uendeshaji, mafunzo, ujenzi wa ofisi, posho za wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji na madiwani.

"Tusitengenezeane fitina za kisiasa kwa jambo ambalo linawezekana kwa kudhani mishahara na posho ya madiwani inapaswa kutolewa na serikali kuu na kama haina uwezo isijibu suala hilo, fedha hazikusanywi, madiwani wanapaswa kuwa chachu, turejesheni kodi ya majengo, tuwekeeni malengo," alisema.

Aliongeza kuwa kuwapo kwa fedha hizo, kutajenga ofisi za ghorofa, zitanunua magari, watalipana posho na kuna kata na mitaa wananchi wataacha kutozwa Sh. 1,000 ya barua.

**TOZO YA VING'AMUZI**

Kuhusu utaratibu unaopendekezwa na serikali wa kutoza Sh. 1,000 hadi 3,000 kwenye ving'amuzi, mbunge huyo alisema: "Hivi vikodi vidogo vidogo mara kwenye ving'amuzi, mtu keshachoka, katumika siku nzima, anarudi nyumbani anataka kuangalia mpira, anakutana na kodi, tutengeneze mazingira rafiki ya kodi kwa wananchi."

# Wakaguzi wa Ndani wasifu mapendekezo bajeti ya serikali

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Ukaguzi wa Ndani Tanzania (IIA) imeipongeza serikali kwa mabadiliko makubwa iliyopanga kuyafanya kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 ili kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani.

Jijini Dar es Salaam jana, Rais wa IIA, Zelia Njeza, alisema hatua hiyo ni kubwa kwa serikali na inakwenda kuongeza ufanisi zaidi kwenye sekta ya ukaguzi wa ndani.

"Kwanza; tunaipongeza serikali kwa kupeleka mapendekezo haya ya kutaka kufanya mabadiliko makubwa kwenye fani ya wakaguzi wa ndani, ambayo yanaanzia kufanywa kwa kuki-boresha Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani," alisema.

Njeza mwenye kiwango cha CPA katika uhasibu na Mwenyekiti wa Bodi ya IIA, alibainisha kuwa taasisi hiyo inaamini mapendekezo hayo yakipitishwa, umma utarajie ufanisi mkubwa, pia kuboresha utawala bora na kupungua vitendo vya ubadhirifu wa fedha.

"Wananchi wategemee kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji na utawa bora, hasa katika matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo, eneo ambalo limekuwa na changamoto kidogo hapo awali," alifafanua.

Alitoa rai kwa wakaguzi wa ndani kujipanga katika utendaji ili kuiunga mkono serikali katika mabadiliko makubwa ambayo imedhamiria kuyafanya katika sekta hiyo.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alipowasilisha bungeni mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka 2022/23 Jumanne wiki hii, alisema serikali imepanga kuimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani kwa kuvijengea uwezo wa kitaaluma na kuongeza idadi ya watumishi katika fani mbalimbali kama vile TEHAMA, uhandisi, ukadiriaji majenzi, wakemia, wanasheria na fani zingine ili kuondokana na dhana ya wakaguzi wa ndani kuwa na taaluma ya fedha pekee.

Waziri Nchemba pia alisema serikali itafanya marekebisho ya Kanuni za Fedha za Umma kwa kuziwezesha Kamati za Ukaguzi kuwa na wajumbe wa nje watatu ikiwamo Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi ili kuongeza uhuru na ufanisi wa kamati za ukaguzi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2022.

Waziri huyo pia alipendekeza Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali kuwa na fungu lake na kuongeza idadi ya wakaguzi wa ndani ili kuimarisha na kuboresha ufanisi katika utendaji.

# Wamiliki wa shule, vyuo wateta na waziri kuondoa kodi ya pango

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekutana na wamiliki wa shule na vyuo visivyo vya kiserikali kujadili kuhusu kuondolewa kwa kodi ya pango la ardhi kwa shule na vyuo hivyo.

Shirikisho la Wamiliki wa Shule na Vyuo visivyo vya kiserikali (TOMONGSCO) liliwasilisha hoja kwa waziri huyo kutaka kuondolewa kwa kodi ya pango la ardhi kwa hoja kuwa vinatoa huduma kama zinavyofanya shule za serikali.

Wakiwasilisha hoja zao mbele ya Dk. Mabula juzi jijini Dodoma, wamiliki hao walisema ni vizuri nao wakatambulika kama taasisi zinazoisaidia serikali katika kutoa huduma ya elimu badala ya kutazamwa kama wafanyabiashara.

Katibu Mkuu wa TOMANGSCO, Benjamin Maduhu, alisema gharama zinazotumiwa kuhudumia wanafunzi wa shule na vyuo hivyo ni kubwa ukilinganisha na ada zinayolipwa na wazazi na kuiomba serikali kuangalia namna bora ya kuwaondolea kodi ya pango la ardhi.

"Waziri gharama za kodi ya pango la ardhi kwa shule na vyuo vyetu ni kubwa tunakuomba utusaidie iondolewe maana tunateseka sana na kuna wakati tunafikiria kubadilisha hata matumizi ziwe hoteli," alisema Maduhu.

Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msavatavangu, ambaye pia ni mmiliki wa shule, alisema: "Serikali iangalie namna gani ya kutuondolea hii kodi ya pango la ardhi maana shule na vyuo visivyo vya kiserikali vinatumia gharama kubwa kuziendesha na 'return' yoyote ikianza kurudi basi ni almost ten years (miaka 10) na baada ya hapo majengo yanahitajika."

Akijibu hoja za wamiliki hao, Dk. Mabula alisema ni lazima zipitiwe kwa kina na wataalamu kuona zilizo za msingi, kuangalia sheria na kama upo umuhimu wa kuiondoa kodi hiyo kutokana na maombi yaliyowasilishwa kwenda kupunguza kodi ya serikali huku akisema lina mchakato mkubwa.

"Najua hamshindwi kulipa kodi ya ardhi bali siyo vipaumbele kwenu na ingekuwa kodi hiyo inaingizwa kwenye bili ya umeme au maji mgelipa.

"Sisi hatuna uwezo wa kuwabana, aidha mgelipia kwa wakati kodi hii wala msingehisi maumivu na mnaona ugumu kwa kuwa mmelimbikiza madeni na mtu anatakiwa kulipa milioni 10 anaona kubwa," alisema Dk. Mabula.

Alisema kuwa anachoweza kufanya kwa sasa kuhusu suala hilo ni kuzungumza na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuangalia namna ya kuwaondolea riba kwa wale wanaodaiwa ili walipe kodi ya msingi na kuwataka wamiliki wanaodaiwa kulipa kodi ya pango la ardhi.




Kaimu Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano ya Vodacom Tanzania Plc, Christina Murimi (katikati), akipokea tuzo ya kampuni bora ya mawasiliano ya simu kwa mwaka 2021 kutoka kwa Ofisa Uendeshaji wa Serengeti Bytes, Michael Mallya jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, ambapo kampuni hiyo, ilishinda kutokana na huduma bora za kidigitali kwa wateja, ambazo ni matokeo ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Vodacom. Kushoto ni Meneja wa Chaneli za kidijitali na malipo kwa mtandao wa M-Pesa, Josephine Mushi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mahakama yawaachia huru wafanyakazi NEMC

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru wafanyakazi wawili wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka ya kughushi, baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Wafanyakazi hao ni Deusdedith Katwe na Magoli Matiku, ambao mbali na shtaka la kughushi pia walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kuwasilisha nyaraka ya kughushi na kuisababishia mamlaka hasara.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi wa Mahakama hiyo baada ya kupitia sheria, ushahidi wa mashahidi zaidi ya 10 wa upande wa Jamhuri na vielelezo mbalimbali.

"Jukumu la kuthibitisha mashitaka dhidi ya washtakiwa ni kazi ya Jamhuri, kwa sababu wameshindwa kufanya hivyo, ninawaachia washtakiwa wote wawili," alisema Hakimu Shaidi.

Kutokana na hukumu hiyo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), iliwasilisha kusudio la kukata rufani Mahakama Kuu kupinga hukumu hiyo dhidi ya washtakiwa hao.

Inadaiwa kuwa kati ya Juni Mosi, 2016 hadi Julai 30, 2017 katika maeneo tofauti ya Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma, washitakiwa hao walikula njama ya kutenda kosa la kughushi, kuwasilisha nyaraka za kugushi na kuisababishia mamlaka hasara.

Ilidaiwa kati ya Agosti 1 hadi Septemba 6, 2016 Katwele alitengeneza nyaraka ya kughushi ambayo ni Ripoti ya Tathmini ya eneo la mradi ya kituo cha mafuta cha Ibra General Enterprise katika kiwanja namba 232 kitalu 'T' eneo la Chadulu 'A' Dodoma.

Kwamba alighushi nyaraka kwa lengo la kuonyesha ripoti ya ukaguzi wa mazingira kwa mradi tajwa ulifanyika wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa kwamba Julai 7 mwala 2016 na Julai 1 mwaka 2017 alighushi muhtasari wa kikao cha kamati ya ushauri wa kitaalamu na kisha kuwakilisha nyaraka hizo kwa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC.

Mshitakiwa Matiku ilidaiwa kwamba Julai 5 mwaka 2016 katika ofisi za NEMC Dar es Salaam, aliwasilisha risiti ya kughushi ya Julai 5, 2016 kwa lengo la kuonyesha ni halali imetolewa na NEMC wakati akijua si kweli.

Ilidaiwa kwamba kwa nyakati tofauti kati ya Juni Mosi mwaka 2016 hadi Julai 30, 2017, eneo la Kinondoni, washtakiwa hao, wakiwa watumishi wa Umma (NEMC), kwa makisudi walikiuka sheria ya baraza hilo na kujipatia Sh. milioni 18.5 kutoka Yunus Mfulla kwa manufaa yao.

Washtakiwa hao pia walikuwa wakikabiliwa na shtaka la kuisababishia NEMC hasara ya Sh. milioni 18.5.

# Talaka zatajwa tatizo ukatili kijinsia nchini

**Na Mary Geofrey**

KUONGEZEKA kwa talaka kwa wanandoa kumetajwa kama moja ya sababu ya zinazochangia kukithiri kwa matukio ya ukatili kwa watoto nchini.

Ofisa wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia Kituo cha Polisi Tabata, Rajabu Ally, alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Taasisi ya Women Tapo.

Alisema wazazi wamekuwa wakichukulia suala la kuachana kama ni mtindo mzuri wa maisha unaofaa ndani ya jamii lakini madhara makubwa wamekuwa wakipata watoto wao.

"Wanandoa wameona kuachana ni fasheni, lakini hawaangalii ni madhara gani wanapata watoto, wanakosa malezi ya kuelewekea, wanatangatanga na kikubwa watoto wote hawapo tayari kuona wazazi wao wanaachana," alisema Ally.

Alisema matukio hayo hupungua wakati wanafunzi wanapokuwa shuleni, wanapofunga shule huongezeka kwa kasi na sababu kubwa ikiwa ni kukosa malezi na uangalizi wa wazazi wanapokuwa mtaani.

Alishauri wazazi kutimiza wajibu wao kuwalea watoto kwa kushirikiana, hasa wanapokuwa nje ya mazingira ya shule ambako kunaonekana hakuna uangalizi wa kutosha.

Ofisa Mipango wa Women Tapo Tabata, Lulu Nyapili, alisema sababu ya kuongezeka kwa matukio hayo ni jamii kuwa na elewa wa kutosha wa matukio ya kikatili na kuyaripoti.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikisaidia kuchukua taarifa za matukio hayo kwa jamii na kushirikisha vyombo vya dola yakiwamo madawati ya jinsia ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema wamekuwa kusaidia watoto wanajihusisha na wanawake waliopo sokoni kwa kuwapa elimu ya kujitambua ili kuondokana na matukio ya ukatili wa kijinsia na kingono.

Mwanaharakati Mkongwe, Dk. Tina Mbaga, alisema wameadhimisha siku hiyo ili kutoa elimu kwa watoto kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia ili kufungua fahamu zao.

Alisema wanawaelemisha kupinga na kupataza sauti zao wanapoona ishara za matukio ya kikatili wa watoto wenzao au kwenye familia zao.

# Waandamana Ubalozi wa Kenya madai upotoshaji

**Na Mary Geofrey**

KUNDI la Jamii ya Wamaasai kutoka maeneo mbalimbali nchini limeandamana kuelekea Ubalozi wa Kenya nchini kuiomba serikali ya nchi hiyo kuingilia kati upotoshaji unaoendelea kuhusu kuhamishwa kwa wananchi kutoka eneo la Loliondo wilayani Ngorongoro mkoani Arusha kwenda Handeni, Tanga.

Kundi la Umoja wa Wamasai waishio Dar es Salaam, liliandamana jana kuelekea katika ubalozi huo ulioko Oysterbay jijini na kuiomba Serikali ya Kenya kuingilia kati upotoshaji unaofanywa na asasi za kiraia na wanaharakati.

Barua iliyoandikwa na Katibu wa Umoja wa Jamii ya Wamasai, Loishiye Lashilunye, iliyosomwa na kiongozi wa msafara huo, aliyejitambulisha kwa jina la Emmanuel, ilibainisha kuwa upotoshaji huo umelenga kuichonganisha jamii ya Wamaasai na serikali yao, pia kuzorotesha jitihada mbalimbali za makubaliano zilizofikiwa na pande zote mbili.

"Tunaiomba Serikali ya Kenya iingilie kati upotoshaji unaofanywa na asasi za kiraia na wanaharakati katika zoezi la kuhama kwa hiari linaloendelea katika Wilaya ya Ngorongoro pamoja na Tarafa ya Loliondo.

"Tunawaomba ndugu zetu kuhamia kwa hiari wilayani Handeni kwenda kuishi kwa amani katika mazingira salama yenye huduma muhimu za binadamu kama maji, umeme na zahahati," Emmanuel alisema.

Aliongeza kuwa wamekuwa wakiona habari za upotoshaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandaoni vikipotosha kuhusiana na zoezi linaloendelea katika eneo la Loliondo na Handeni.

"Kwa pamoja tunakemea upotoshaji huu kwa sababu siyo tu unaichonganisha jamii na serikali yake bali unarudisha jitihada mbalimbali za maridhiano yaliyofanywa na pande zote mbili," alisisitiza.

Aliendelea kusema kuwa, Serikali ya Kenya inapaswa kufanyia kazi maombi ya umoja huo kwa maslahi mapana ya wananchi, marafiki na jamii ya Wamasai.

Tamko hilo limekuja siku chache baada ya kuwapo kwa upotoshaji baada ya serikali kuweka alama za mipaka katika eneo la Loliondo pamoja na uhamaji wa wananchi wa Ngorongoro kuelekea makazi mapya Handeni.

Kundi la kwanza la wananchi waliokuwa wakiishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, limeshalipwa fidia na kuondoka rasmi juzi kuelekea Tanga kuanza maisha mapya.

Kundi hilo la familia 27 kati ya 103 zilizokubali kuondoka kwa hiyari kwenye hifadhi hiyo, lilipokewa na viongozi mbalimbali katika Kijiji cha Msomera wilayani Handeni juzi.



Rais wa Shirika la Kimataifa kutoka nchi ya Korea Kusini CTS, Kyung Chul Kam (kulia), akisaini mkataba wa makubaliano ya utekelezaji wa miradi ya kijamii na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Zainabu Makwinya, wilayani Arumeru, mkoani Arusha jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo, Jeremia Kishili. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Anna Mkapa afichua siri kuanzisha taasisi

**Na Romana Mallya**

MKE wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, Mama Anna Mkapa, amesema katika kusherehekea miaka 25 ya taasisi isiyo ya kiserikali ya Equal Opportunities For All Trust Fund (EOTF), wamejifunza nchi ina umaskini ambao watu wengi hawaujui na wao ni kama wamedonoa tu kwa kuwa hawawezi kusaidia wote.

Alisema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumzia matukio mbalimbali iliyoyaandaa kusherehekea miaka 25 ya taasisi ya EOTF tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997 ambayo yanatarajia kufanyika ndani ya wiki moja kuanzia keshokutwa.

Akizungumzia walikotoka, Mama Mkapa alisema wakati mume wake, Hayati Rais Mkapa, akiongoza nchi, alipokwenda mkoani kwa programu alizopangiwa, yeye alitembelea maeneo tofauti ikiwamo vituo vya watoto yatima.

"Walio wengi ulikuwa ukiwauliza mnawahudumia (watoto ) namna gani? Wanakueleza 'wanaletwa hapa, wenyeji wakitusaidia chakula tunawapa lakini tunategemea msaada', roho ikaniuma kama wao wanaweza, kwanini mimi nisiweze? Ndivyo nilivyoanzisha hii taasisi hii.

"Lakini, kwa kweli nchi yetu ukitembea mkoani ndipo utakavyojua umaskini ulivyokithiri, watoto wana njaa, wanakwenda shule hawana sare za shule, hawana viatu, shati limechanika, unajiuliza anachokisoma anakielewa? Taasisi ni kama tumedonoa tu, hatuwezi kusaidia wote," alisema.

Mama Mkapa alitoa wito kwa wale ambao wamesaidiwa na taasisi hiyo wasijibweteke, bali nao wawasaidie wengine ili wanufaike wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Stephen Emanuel, alisema baada ya sherehe hizo ambazo kilele chake ni Juni 27, mwaka huu, wamejipanga kujenga kituo kitakachojulikana kama 'Women Business Center' ambacho shughuli zote za wanawake zitaonekana humo na watatafuta biashara na masoko.

Kuhusu sherehe hizo, Emmanuel alisema zinatarajia kuanza Jumatatu ijayo na kufikia kilele Juni 27, mwaka huu.

Alisema dira kuu ya taasisi hiyo ni kusaidiana na serikali kuwawezesha wanawake na vijana wanaoishi katika mazingira duni hasa kutoka vijijini, kupiga vita umaskini, ujinga na maradhi na kujiletea maendeleo yao ya kweli.

Alisema kuwa Jumatatu katika Kituo cha Kimataifa cha Julius Nyerere kutafanyika uzinduzi wa maonyesho ya bidhaa za wanawake wajasiriamali kutoka Tanzania Bara na Visiwani ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"Siku itakayofuata, zitatolewa mada mbalimbali za ujasiriamali, elimu , maradhi, upatikanaji mitaji, stadi za maonyesho ya biashara na uungwanishwaji wa masoko ya bidhaa za wanawake wajasiriamali katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo yatatolewa bure, yatafanyika katika ukumbi mpya wa JKT Mgulani kuanzia saa tatu asubuhi kila siku na yatakwenda sambamba na maonyesho.

Pia alisema kutakuwa na bonanza la mpira wa miguu, ambapo mechi ya ufunguzi ya wanawake wa viongozi na wanawake wasajiriamali itafanyika na baadaye timu ya Simba Queens na Yanga Princess zitacheza Uwanja wa Benjamin Mkapa Juni 25, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa ni Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete.

Alisema mshindi atakabidhiwa kombe kubwa la kifahari linaloweza kushindaniwa tena mwakani na lengo lake ni kuhamaisha wasichana na wanawake kuona michezo ni kazi.

Emanuel alisema Juni 26 mwaka huu, kutakuwa na chakula cha hisani kuchangia EOTF kuendelea na kazi zake, shughuli ambayo itafanyika ukumbi wa Diamond Jubilee na mgeni rasmi anatarajia kuwa ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"Kilele cha sherehe hizi ni Jumatatu (Juni 27,mwaka huu) zitafanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa ni Rais Samia Suluhu Hassan. Siku hiyo kutakuwapo na maonyesho madogo ya bidhaa za wanawake wajasiriamali kutoka Bara na Visiwani Zanzibar.

"Tutawapa tuzo wahisani waliosaidia EOTF tangu mwaka 1997 hadi leo, ushuhuda kutoka kwa waliosadiwa na kuwezeshwa na taasisi katika kila Nyanja utatolewa kwa siku zote za sherehe," alisema.


**STEP MARK**

Makumbusho, PLOT No. 13 Block 45, P.O.Box 11767, Dar es salaam, Tanzania
Office : +255 715 300 312 , E-mail: info@stepmark.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA!!**

**Step mark Limited** kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya CRDB Makao Makuu** yaliopo **Plot Namba. 25&26 Ally Hassan Mwinyi Road & Plot Namba.21.Barack Obama Road, S.L.P 268,11101 Dar es Salaam** tunatangaza minada ya hadhara wa kuuza mali za wadaiwa wa **Benki ya CRDB** sehemu mbali mbali katika mikoa ya Tanzania.

Mali hizo zitauzwa kama zilivyo kwenye eneo kwa njia ya Minada ya hadhara..

| S/No | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI | TAARIFA YA MALI INAYOUZWA | ENEO MALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Israel Delius Mahenge | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa: Mwanyanje Kata: Igawilo Jiji la Mbeya. | 03/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 2. | Joshia Daniel Magabe | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa; Mponja Kata;Igawilo Jiji la Mbeya | 04/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 3. | Gasper Johnson kiando | NYUMBA | Hati namba 89-RUKLR Namba ya makazi 791609 | Ploti namba 383 Block 'T' Mtaa;kisiwani Sumbawanga | 04/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 4. | Apolinary Sipriano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 5. | Apolinary Sipriano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 6. | Apolinary Sipriano Selemani | GARI | Namba ya usajili. T926DBZ Chassis No: MAT382042E7R11237 Aina: LP Aina ya Umbo:BUS Usajili wa kadi: 7812249 | Nkasi | 06/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 7. | Masiwa hardware Supplies limited | GARI | Namba ya usajili. T777DJJ Chassis No:IXGTT10ACGA000604 Aina: TT100A Aina ya Umbo: Trailer Usajili wa kadi: 7658635 | Sumbawanga | 9/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 8. | Bakari Said Mayongo | NYUMBA | Hati namba; 25302-MBYLR Namba ya makazi;381142 | Ploti namba 237, Block 'OO'high dendity Sumbawanga | 12/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 9. | Venus Joseph Ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; sheli Kata; Nchola Wilaya; Namanyere Mkoa;Sumbawanga | 15/07/ 2022 Saa Nne Asubui Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 10. | Venus joseph ruhunyu | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; minsukumilo Kata;kipindu Wilaya; namanyere Mkoa;sumbawanga | 16/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 11. | Friday Samson mziho | NYUMBA | Hati namba; 48063 MBYLR, Namba ya makazi;991835 | Ploti namba 1, Block 'A'medium dendity majengo, Namanyere urban area. | 18/07/ 2022 Saa Nne Asubui Mwisho Saa Kumi Jioni |
| 12. | Paul Phares Mnyandwa | NYUMBA | Hati namba; 2124 Namba ya makazi;1031860 | Ploti namba 413, Block 'V' Unguu Road GAIRO. | 19/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni. |
| 13. | Sawaka Nchola Ganja | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji; matai B Kata; Nchola Wilaya; | 20/07/ 2022 Saa Nne Asubuhi Mwisho Saa Kumi Jioni |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi lazima afike eneo la mnada unapofanyika
2. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano(25%) ya bei iliofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada na mteja akishindwa kulipa 75% ndani ya siku 14 atakua amepoteza haki ya ununuzi.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA 0677 992 040 /0677 992 030**

2169087O2

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars ina mlima mrefu kufuzu Afcon

**TIMU** ya taifa, Taifa Stars, ilishindwa kupata ushindi kwenye mchezo wake wa pili wa kuwania kufuzu kushiriki michuano ya Mataifa ya Afrika, Afcon 2023, baada ya kufungwa mabao 2-0 na Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Stars ilipoteza mchezo huo baada ya awali kutoka sare ya 1-1 dhidi ya Niger kwenye mchezo wa kwanza uliopigwa Cotonou, nchini Benin.

Matokeo dhidi ya Algeria siyo ya kushitua kutokana na kiwango chetu dhidi yao, lakini kwa kuzitazama dakika 90 za mechi hiyo ziliibua mshangao kwa namna mabao yalivyopatikana na mwisho kujikuta tumepoteza mechi.

Pamoja ya kufahamika ujanja walionao wachezaji wa Algeria, ambao wengi wao wanakipiga ligi za Ulaya, lakini Stars ilionesha kumudu angalau kasi na ujanja wao kwa kuuchezea na kujaribu kutafuta nafasi mbele yao.

Hata hivyo, juhudi zote hizo zilikwama kwenye sehemu ndogo ndogo mno zilizohusisha utimamu wa kumudu presha ya mchezo na mbinu chache, ambazo bado mpaka leo ni kikwazo kwenye kikosi hicho cha kocha Kim Poulsen.

Stars ilianza mechi hizi za kufuzu kwa morali kubwa baada ya kupata sare na Niger huku Uganda ikifungwa mabao 2-0 na Algeria.

Lakini sasa mambo yameanza kuwa magumu katika mechi ya pili tu. Mechi ijayo tutaumana na Uganda kwao kisha tutarudiana tena hapa kabla ya kucheza na Niger kisha kuifuata Algeria kwao.

Kimahesabu tunaona kwamba, ni mlima mrefu mno kwa kuwa sasa, mazingira yameshakuwa mepesi kwa Algeria na waliobaki wanawania nafasi moja.

Kuwania nafasi kama hiyo dhidi ya Uganda na Niger si kitu rahisi tena ndani ya mechi nne tu zilizobaki, bado tunahitaji kuongeza umakini kwenye makosa madogo madogo yanayotugharimu kiasi hiki.

Stars inapaswa kujiamini na kufahamu ushindani ni ushindani pasipo kuwa na busara zisizo na msingi wala kuzubaa hata kidogo. Kuna muda mpira unakupa matokeo kwa mbinu tu na si ujuaji wa kuuchezea mpira sana.

Tunachotakiwa kufanya ni kuongeza mbinu na umakini, wachezaji wajitambue wanapopewa majukumu, kujitoa na kucheza na kuzingatia bahati zinazotokea ndani ya dakika 90 ni suala la msingi pia.

Kilichopo mbele yetu kwa sasa ni kuhakikisha kwamba, Stars inaimarika vizuri zaidi kwenye mazoezi ili mechi zinazokuja ziwe kwa ajili ya kutafuta ushindi tu na sio sare.

Ni wazi kwamba, sasa zimebaki timu tatu kwenye kundi letu ambazo zinagombea nafasi moja, hivyo kazi ni kubwa mno kwa Stars kuweza kuupanda mlima huu, lakini kila kitu kinawezekana, tukiamua na kujidhatiti kwa nguvu moja.


Sisi tunashauri kwamba, benchi la ufundi kwa sasa linatakiwa kukaa chini kufikiri na kutafakari hizi mechi zilizobaki za Stars inaingiaje uwanjani, kwani tukipoteza mchezo unaofuata ni wazi nafasi ya kufuzu itakuwa finyu mno kwetu.

Sasa kazi iliyopo mbele yetu kwa sasa ni kuhakikisha kwa namna yoyote ile angalau tupate ushindi kwenye mechi mbili kati ya nne zilizobaki huku tukiombea maumivu kwa wapinzani wetu waweze kupoteza kwenye mechi zao.

Hapo angalau tunaweza kuwa na uhakika wa kufuzu, kwani bila kujali matokeo ya wapinzani wetu, tutakuwa tumejihakikisha pointi saba kibindoni ambazo kwa namna fulani zinaweza kutusaidia kufuzu kwenda kwenye Afcon ambapo itakuwa mara yetu ya tatu katika historia baada ya kufanya hivyo kwa mara ya kwanza mwaka 1980.

Wito wetu kwa sasa, wadau viongozi na wapenzi wote wa soka kuungana pamoja katika kuhakikisha kwamba, Stars inapata nafasi ya kufuzu Afcon ili kuweza kulitangaza soka letu kimataifa na kuendelea kunyanyuka kwenye orodha ya viwango vya ubora vya Shirikisho la mpira wa miguu duniani, FIFA.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongereni Yanga, ila jipangeni kimataifa

**HII** ni mara ya 28 kwa klabu ya Yanga kutwaa Ubingwa wa Tanzania Bara. Jumatano iliyopita, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walipata furaha isiyo kifani baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa kwa kuifunga Coastal Union mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikifikisha pointi 67 ambazo haziwezi kufikiwa na timu yoyote ile.

Wanachama na mashabiki wa Yanga waliusubiri ubingwa huo kwa misimu minne ambapo ni kama ulikuwa umehamia kwa watani zao wa jadi, Simba.

Baada ya dhiki faraja, unaweza kusema hivyo, kwani ilipitia kipindi kigumu, lakini viongozi, wanachama na mashabiki walikuwa wavumilivu na kupambana kuhakikisha wanairudisha timu kwenye hali ya ushindani.

Walichofanya kabla ya msimu huu ni kusajili kikosi ambacho kimekuja si tu kuleta ushindani kwenye Ligi Kuu bali kuwa tishio.

Hadi kinachukuwa ubingwa bado hakikuwa kimepoteza mechi yoyote ile na mpaka sasa timu hiyo imesalia mechi tatu ili iweze kuweka rekodi ya kucheza msimu mzima bila kupoteza.

Pamoja na kufanya usajili wa wachezaji wengi, lakini uliowezа kuwafanya kuwa tishio na kuwapa ubingwa ni wa kipa Djigui Diarra wa Mali, Yannick Bangala, Mayele, Djuma Shaaban na Jesus Moloko kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Khalid Aucho kutoka Uganda.

Kwa hakika wachezaji hawa wakichanganyika na wengine waliowakuta na wachache waliosajiliwa kutoka klabu mbalimbali hapa nchini ndiyo kwa kiasi kikubwa waliofanya Yanga kuwa timu isiyoshindika.

Nitoe pongezi kwa viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hiyo ambao kwa pamoja wameiwezesha timu hiyo kutwaa ubingwa msimu huu, ikiwa ni mara ya 28 tangu kuanza kucheza ligi nchini Tanzania mwaka 1965.

Hata hivyo, ukweli lazima usemwe kuwa pamoja na kwamba Yanga ndiyo timu iliyotwaa ubingwa mara nyingi nchini Tanzania, lakini rekodi yake kwenye michuano ya kimataifa hairidhishi hata kidogo.

Imekuwa ikijitutumua mara kadhaa, lakini imekuwa ikiangukia pua, wakati mwingine mechi za awali, raundi ya kwanza au ya pili.

Ina rekodi nzuri ya kuwa ndiyo timu ya kwanza kuingia hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 1998, lakini hata hivyo haikushinda mechi yoyote.

Hapa nazungumzia michuano ambayo inakwenda kushiriki ya Ligi ya Mabingwa na si Kombe la Shirikisho.

Ni miaka 24 sasa Yanga haijaweza kutinga tena hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika licha ya kuwa kuna wakati ilikuwa na kikosi madhubuti ambacho kilitakiwa kiwe kimeingia kwenye hatua hiyo.

Achana na kikosi cha kina Bernard Mwalala, au Boniface Ambani na wala sitaki kuizungumzia Yanga bora kabisa kuwahi kutokea Tanzania ya miaka ya 1980, ngoja tukizungumzie kikosi cha mwaka 2014 mpaka 2015.

Nadhani Yanga ilikuwa na kikosi bora zaidi naweza kusema kuliko hiki, lakini hakikuweza kutinga hatua hiyo, hivyo hapo viongozi wanaweza kuanzia, waangalie tatizo lilikuwa nini ili waanze kuliangalia na kulirekebisha mapema.

Kuna wakati kikosi cha Yanga kiliundwa na Deogratius Munishi 'Dida', Juma Kaseja, Mbuyu Twite, Oscar Joshua, Nadir Haroub 'Cannavaro', Kelvin Yondani, Frank Domayo, Simon Msuva, Haruna Niyonzima, Emmanuel Okwi, Mrisho Ngassa, Hamisi Kiiza, Juma Abdul, David Luhende, Athumani Idd 'Chuji', Hassan Dilunga, Said Bahanuzi, Didier Kavumbavu na wengine.

Hebu pata picha, kikosi kama hiki bado kilishindwa kutinga hatua japo ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa misimu miwili mpaka mitatu hadi kilipoanza kupanguka tena. Hapa kuna tatizo.

Ina maana viongozi wa Yanga hawakukaa tena vizuri na akili yao kuelekeza kwenye michuano ya kimataifa, hata kikosi hiki kinaweza kutolewa.

Hapa inaonyesha tatizo halipo kwenye timu, bali viongozi. Labda kwa sasa ambapo uongozi unakwenda kubadilika. Ni aibu kwa zama hizi kwa timu za Simba na Yanga kuwekeza nguvu kubwa kwenye kutwaa ubingwa wa bara, huku zikishindwa kutinga hata hatua ya makundi. Kwa sasa naona Simba imeanza kujipambanua.

Simba na Yanga ni timu za zamani sana na zimechelewa sana kujua kimataifa ndiko kunalipa.

Kinachotakiwa sasa Yanga ni kuacha kuchukua muda mrefu kusherehekea ubingwa kwani hiyo kwake si mara ya kwanza, bali kujiandaa sasa na michuano ya kimataifa ambayo kwake imekuwa mwiba mchungu.

Tuliona msimu uliopita timu hasimu za Sudan, Al Hilal na El Merreikh zikiwa kundi moja kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Hivyo ndiyo Watanzania wengi wanahitaji na si miaka nenda rudi kupigiana kelele humu humu ndani na kuzifunga timu dhaifu, wakati mwingine kwa msaada wa makocha na waamuzi.

Tunataka kuziona Simba na Yanga zote zikitinga makundi Ligi ya Mabingwa msimu ujao kwa kuziandaa timu zao kikamilifu na viongozi hasa wa Yanga kuwa na dhamira ya dhati kwenye michuano hiyo.

## Serikali mbioni kukamilisha mapitio gharama za bandari

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho kufanya mapitio ya gharama za huduma za bandari kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kabula Shitobela.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itapunguza tozo zinazotozwa na TPA kwa kuwa imekuwa ikitoza tozo kubwa kwenye mizigo kuliko kampuni binafsi ili kuendana na ushindani wa soko.

Akijibu swali hilo, Mwakibete alisema lengo ni kuhakikisha bandari zote zinatoa huduma bora kwa gharama nafuu ili kuendana na hali halisi ya ushindani katika bandari za ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

"Hivi sasa uchambuzi wa maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali yanafanyiwa kazi na zoezi hili linatarajiwa kukamilika Julai, 2022," alisema.

## Kanuni za Uvuvi sasa kufumuliwa

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kufanya marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2020 ambazo zinalalamikiwa na wadau.

Ulega alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Kilwa Kusini (CCM), Ally Kasinge, aliyetaka kujua lini serikali itafanya marekebisho ya kanuni hizo.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema marekenisho hayo yatakamilika Julai mwaka huu.

Alifafanua kuwa serikali kupitia wizara hiyo inaendelea kufanya marekebisho ya kanuni hiyo ili kuboresha shughuli za uvuvi nchini na biashara ya mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi.

"Kwa kuzingatia maoni ya wadau wa sekta ya uvuvi na maoni yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwenye vikao kati ya wizara na kamati hiyo vilivyofanyika Machi 30, 2020 na Agosti 25, 2021, marekebisho ya kanuni husika yanatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022," alisema.

# Bilioni 60/- zakusanywa tozo Daraja la Nyerere

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Mei mwaka huu, Mfuko wa NSSF umekusanya Sh. bilioni 66.86 kutokana na tozo kwa watumiaji wa Daraja la Nyerere lililoko Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Kigamboni (CCM), Dk. Faustine Ndugulile.

Mbunge huyo alihoji kiasi cha fedha kilichokusanywa tangu Daraja la Nyerere lianze kutumika na mpango wa serikali kufanya huduma ya daraja hilo kuwa bure.

Naibu Waziri Kasekenya, akijibu swali hilo, alisema mfuko huo ulianza kupokea fedha zitokanazo na tozo kwa watumiaji wa Daraja la Nyerere mnamo Mei 14, 2016 baada ya kuzinduliwa.

"Serikali imeendelea kupunguza tozo kwa watumiaji wa daraja hilo tangu kuzinduliwa kwake kwa kuzingatia tathmini ya uwezo wa wananchi kumudu tozo hizi. Kwa mara ya mwisho serikali imepunguza tozo husika Mei 21, 2022"alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaanza mchakato wa kutoza tozo hizo kwa siku, wiki na mwezi kama zimeshapunguzwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kasekenya alisema kwa sasa mfumo wa kufanya hivyo unakamilishwa na ifikapo Julai Mosi mwaka huu utaanza kutumika.



Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima, akiuliza swali la nyongeza kwenye kipindi cha maswali wakati wa mkutano wa saba kikao cha 46 cha Bunge la Bajeti, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ahoji vigezo kuanzisha kituo polisi

MBUNGE wa Donge (CCM), Soud Mohammed Jumah, amehoji vigezo vinavyotumika kwenye uanzishwaji vituo vya polisi nchini.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alihoji serikali inatumia vigezo gani kuanzisha vituo vya polisi katika maeneo ambayo idadi ya watu na vitendo vya uhalifu vinaongezeka.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alifafanua kuwa vigezo vinavyotumika kuanzisha vituo vya polisi ni ongezeko la watu na ongezeko la matukio ya uhalifu.

Alitaja vigezo vingine ni umbali kati ya kituo kimoja cha polisi na kingine, uwapo wa miundombinu ya serikali, shughuli za kibiashara pamoja na maeneo ya kimkakati kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi, uwezo wa kibajeti na utayari wa wananchi na Mamlaka zao za Serikali za Mitaa.

Alibainisha kuwa hatua inayofuata ni mapendekezo ya uanzishwaji wa kituo husika kuwasilishwa kwenye Kamati ya Usalama ya Wilaya, Mkoa na kisha ushauri wao huwasilishwa kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa ajili ya utekelezaji.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Watumiaji wa M-Pesa kupata gawio bil. 3.3/-

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya mawasiliano ya simu ya Vodacom Tanzania Plc, imeanza kutoa mgao wa Sh. bilioni 3.3 kwa watumiaji wake zaidi ya milioni 7.7 ikiwa ni sehemu ya faida iliyopatikana kwenye akaunti za M-Pesa.

Malipo hayo yanategemewa kukamilika Juni 17 na wateja wote watakuwa wameshapokea mgawo wao na kufanya idadi itakayotolewa kwa ujumla kufikia Sh. bilioni 174 tangu kampuni hiyo ianze kugawa faida kwa wateja wake.

Akifafanua kuhusu gawio hilo, Mkurugenzi wa M-Pesa Epimack Mbeteni, alisema: "Tuna furaha kubwa kuona kuwa huduma ya M-Pesa inaendelea kuwa msingi wa shughuli za kibiashara pamoja na maisha ya kila siku ya wananchi nchini.

"Tuko katika mchakato wa kugawa Sh. bilioni 3.3 kwa wateja wetu ambao wamekuwa wakitumia mfumo wetu kwa kipindi hiki na malipo yanaingia moja kwa moja katika akaunti zao za M-Pesa."

Alisema faida italipwa kwa wateja, mawakala, wakala mkuu na wadau wengine wa kibiashara wa M-Pesa kulingana na matumizi yao ya huduma za M-Pesa.

Alisema gawio linategemea kiasi cha matumizi ya huduma katika kipindi hicho cha robo ya kwanza ya mwaka 2022 (Januari hadi Machi). Shughuli hizo ni pamoja na kuhamisha pesa, kulipa bili, manunuzi ya muda wa maongezi na mengine.

Mbeteni aliongeza: "Mfumo huu wa kipekee umekuwa na nafasi kubwa katika kujenga hali ya ushirikishwaji na upatikanaji wa huduma za kifedha nchini. Wanawake na vijana wameona unafuu na urahisi wa kutumia M-Pesa na wanatumia huduma nyingi ili kuboresha maisha yao.Mfumo umekuwa rasilmali muhimu katika kuwezesha biashara ndogondogo na kupambana na changamoto zilizosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO -19."



Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa kampuni ya usambazaji wa matairi ya magari makubwa na madogo ya Superdoll, Adam Mubago (kulia), akitoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya magurudumu kwa madereva wa mabasi ya mikoani na nchi za jirani, katika kituo cha Magufuli, Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mramba akunwa India kuwekeza Tanzania

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, amesema maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa sasa ni kuifungua Tanzania kwa kuwakaribisha wawekezaji katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi.

Alisema kampuni za uwekezaji kutoka India zilizokuja nchini kwa fursa hiyo, zimeonyesha utayari wao kufanya biashara na Watanzania.

Mramba aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano uliowakutanisha wawekezaji kutoka India na Tanzania wanaojihusisha na biashara katika maeneo ya umeme, vifaa vya umeme na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ili kujadiliana.

Mkutano huo uliandaliwa kwa ushirikiano baina ya Ubalozi wa India nchini pamoja na Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Akifungua mkutano huo, Mramba alisema kuifungua nchi kuna maana nyingi -- kutoa nafasi ya mitaji kuingia katika nchi, kubadilisha teknolojia na kuileta ya kisasa na kukuza ujuzi wa Watanzania.

"Kampuni hizi za India tunazoziona leo zimekuja kwa uwekezaji, zipo tayari kuwekeza hapa, zipo tayari kufanya biashara na miongoni mwa maeneo ambayo wanayaangalia ni umeme, vifaa vya umeme na ICT.

"Wawekezaji hawa wapo tayari kufanya kazi na Watanzania. Sekta ya Nishati ni miongoni mwa sekta zilizonufaika na ushiriki wa wafanyabiashara wa India kwa miaka mingi, tumekuwa tukipata vifaa vya umeme, transfoma na waya. Miongoni mwa nchi zilizopiga hatua eneo hili la vifaa hivi ni India," alisema.

Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, alishukuru TCCIA kwa kushirikiana nao kwa sababu wamekuwa wakipata msaada katika maeneo mbalimbali hasa wafanyabiashara wao wanapokuja Tanzania kuangalia fursa za uwekezaji na biashara.

Alisema kwa mara ya kwanza, India imefanikiwa kufikia Dola za Kimarekani bilioni 4.5 kwa mwaka 2021/22 kutokana na ukuaji wa biashara kati ya nchi hizo.

Alisema kulingana na takwimu, mauzo ya bidhaa India kwenda Tanzania ni asilimia 59.89 na uagizaji kutoka Tanzania katika kipindi hicho 2021/22 ni asilimia 143.79.

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alisema wao pamoja na Ubalozi wa India wamekaa na kupokea ujumbe wa kibiashara wa sekta ya ICT ambayo kwa sasa ni eneo muhimu.

"Wote tunafahamu umuhimu wa ICT, leo (juzi) tunaweza kufanya kazi dunia nzima kupitia mtandao bila kusafiri, ukiwa nyumbani kwako mambo mengi sasa yanawezekana kabla hujapanda gari na kuchafua hali ya hewa," alisema.

Katika majadiliano, pande zote mbili wamekubaliana kuendelea kuimarisha ushirikiano kati ya nchi hizi mbili katika sekta mbalimbali ikiwamo kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika sekta nyingine pia kama ya afya, uendelezaji wa bandari na ya kilimo.

# Mchumi wa WB aipongeza TASAF kutekeleza mpango

**Na Elizabeth Zaya,** BAGAMOYO

MCHUMI Mwandamizi kutoka Benki ya Dunia (WB), Michele Zini, ameupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa namna unavyoratibu na kutekeleza mpango wa kunusuru kaya maskini na hivyo kuleta matokeo chanya kwa wanufaika.

Mchumi huyo alitoa kauli hiyo katika ziara ya kuwatembelea na kuzungumza na walengwa wa mpango huo katika kijiji cha Matimbwa kilichoko Bagamoyo mkoani Pwani iliyohusisha wajumbe kutoka Uswisi, Benki ya Dunia na Norway.

Alisema utaratibu uliowekwa na TASAF katika kutekeleza mpango huo ndio umechangia kuufanikisha kwa kiwango kikubwa na kuleta matokeo hayo chanya.

"Katika ziara hii ya kutembelea na kuzungumza na walengwa wa mpango huu wa kunusuru kaya masikini, tumejifunza mambo mengi na kikubwa zaidi ni namna ambavyo TASAF inaratibu na kutekeleza mpango, huu utaratibu ni mzuri na ndio maana umefanikiwa na kuleta matokeo chanya kwa hawa wanufaika.

"Ni jambo zuri sana kuona walengwa wanafundishwa taaluma ya namna ya kuanzisha na kuendesha miradi ya kujiongezea na kujikomboa kiuchumi.

"Tumeshuhudia hapa vikundi vya walengwa vikiwa na miradi yao ya biashara, wametuonyesha namna wanavyotumia ruzuku yao wanayopewa, pesa yoyote wanayoipata wanahakikisha wanaitumia kwa malengo na siyo kwa ajili ya starehe, hili ni jambo zuri sana, tunapongeza TASAF kwa utaratibu na usimamizi mzuri," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Bagamoyo, Shauri Selenda, alisema mpango huo wa kunusuru kaya maskini umesaidia kuinua kipato kwa walengwa hususani kupitia miradi yao midogo midogo wanayoianzisha baada ya kupata ruzuku.

"Halmashauri yetu tunaishukuru sana TASAF kwa sababu imewakomboa wananchi wetu kwa kiwango kikubwa, sasa hivi familia zinaishi maisha bora, zimeboresha makazi yao, zina uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku na zimeanzisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato.

"Walengwa wameanzisha vikundi vya kujiwekea akiba na wamekuwa wakikopeshana kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi na biashara zao mbalimbali.

"Wapo walengwa ambao wamejikita kwenye kilimo, wengine wanafuga, mama lishe, wanauza nguo, vyombo na shughuli nyinginezo, na hili limechangia kwa wao kuwa na nidhamu ya kutunza na kuwa na matumizi mazuri ya fedha," alisema.

Mkurugenzi wa Programu za Jamii TASAF, John Stephen, alisema wataendelea kuongeza nguvu zaidi ya kutoa elimu kwa walengwa hao juu ya matumizi bora ya ruzuku wanayowapatia, namna ya kubuni na kuanzisha miradi mbalimbali pamoja na kuisimamia ilete matokeo chanya.

"Hatutawakatia tamaa, hata baadhi yao ambao wakati mwingine wanapata changamoto ya kuanzisha miradi, tutahakikisha tunaongeza nguvu kuwapatia elimu ili wajikomboe kiuchum,"alisema Stepheni.



# Jamii inahitaji kushirikishwa matibabu saikolojia - Ripoti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na madaktari bingwa wa magonjwa ya afya ya akili, umebaini jamii inahitaji ushirikishwaji wa matibabu ya kisaikolojia ili kuepuka matukio mbalimbali yanayofanywa ikiwamo mauaji kwenye familia.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa ya Mirembe, Dk. Paul Lawala, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari katika warsha ya wataalamu wa afya iliyofanyika katika ukumbi wa hospitali hiyo.

Dk. Lawala alisema utafiti huo umefanywa ndani ya miaka mitatu na madaktari hao katika Hospitali ya Taifa Muhimbili pamoja na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya na kuleta matokeo chanya kwa wagonjwa waliofanyiwa kwa kushirikisha jamii.

"Huu ni utafiti mdogo wa awali uliofanywa na madaktari bingwa wa afya ya akili na utafiti huu utatumika kama mwongozo wa utafiti mkubwa uliopangwa kufanyika mwakani katika mikoa mitatu," alisema Dk. Lawala. Alisema lengo la kufanya utafiti huo ni pamoja na kutaka kuthibitisha kama ushirikishwaji wa jamii katika matibabu ya kisaikolojia unahitajika kwa kiasi kikubwa kwa wagonjwa ili wapate kupona.

Akizungumzia kuhusiana na matokeo chanya, alisema wamebaini jamii yenye wagonjwa ikishirikishwa wenye matatizo hayo wanapata nafuu na wengine wanapona kabisa.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alisema mwakani wamepanga kufanya utafiti katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma ambapo zaidi ya vituo 20 vitashiriki katika utafiti huo.

Alisema pia watu wa tiba asili, viongozi wa dini na jamii nao watajumuishwa kwa lengo la kutoa elimu ya kisaikolojia ambayo inasaidia kwa wagonjwa.

Alisema sababu ya kuchagua mikoa mitatu kufanya utafiti mkubwa wa afya ya akili ni kutokana na kuwa na vifaa na miundombinu kwa ajili ya kufanyia utafiti.

Dk. Praxeda Swai kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alisema neno KUPAA linamaanisha kupata uzima ikiwamo kupata elimu ya kisaikolojia kwa wagonjwa wa afya ya akili pamoja na familia.

Alisema tiba hiyo inawasaidia wagonjwa kupona na kuanza kufanya shughuli zao za kijamii za kila siku pamoja na jamii nyingine.

"Hii tiba ni nzuri sana na inatumika katika mataifa mbalimbali, Tanzania itakuwa ya kwanza kuanza kuitumia baada ya kufanyiwa utafiti," alisema Dk. Swai.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (katikati), akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment, Dk. Fred Msemwa (kulia), baada ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa nyumba, eneo la Kisasa Njedengwa, jijini Dodoma jana. **PICHA: UTUMISHI**

# RC aonya vituo bodaboda kugeuzwa maficho ya uhalifu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Athony Mtaka, aliwaonya madereva bodaboda kutovitumia vituo vyao kama sehemu ya kujificha kufanya vitendo viovu.

Mtaka alitoa onyo hilo jana alipozungumza na wenyeviti na makatibu wa waendesha bodaboda na bajaji wa Jiji la Dodoma.

Onyo hilo linakuja baada ya kuwapo taarifa kutoka kwa wananchi kuwa kuna waendesha bodaboda na bajaji wanajihusisha na vitendo vya kihalifu kupitia vyombo vyao vya usafiri. Alisema kazi ya bodaboda lazima iheshimiwe kama zilivyo kazi zingine na ndiyo maana watu wengi wanatumia usafiri huo ambao ni rahisi.

"Ninataka kuwatangazia wale wote waliojificha kwa kivuli cha udereva wa bodaboda na bajaj wakati vitendo vyao ni viovu, wajiondoe mapema kabla ya kuwabaini maana jela haitawaacha," alionya.

Mtata aliwataka madereva hao kuithamini kazi yao kwa kuwa ni sehemu ya kujipatia kipato na kutatua shida mbalimbali kwenye maisha yao ya kila siku.

Aliwakumbusha kuzingatia sheria na kanuni za barabarani za uendeshaji wa bodaboda na bajaj walizonazo, ili kuepuka kamata kamata inayofanywa na vyombo vya dola.

Mwenyekiti wa Mkoa wa Waendesha Bodaboda, Keneth Chimoti, alisema wataendelea kuwafichua wale wote wanaochafua kazi hiyo ya bodaboda kwa kufanya vitendo viovu vya kihalifu.

"Taarifa na vitendo vinavyofanywa na baadhi yetu vinaichafua serikali yetu ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anatuamini kwa kuwa tunafanya kazi ya kujiajiri wenyewe," alisema.

Aliongeza kuwa madereva bodaboda wataendelea kutoa ushirikiano kwa serikali na kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni ili kuondokana na kukimbizana na polisi kwa hofu ya kukamatwa.

Alisema kazi wanayoifanya wengi wao wameweza kupata mafanikio na kumudu kuendesha maisha yao kama vile kusomesha watoto wao.

## Kamati za ulinzi mtoto zaundwa

**Na Renatha Msungu,** BAHI

WILAYA ya Bahi mkoani Dodoma imeunda Kamati za Ulinzi na Usalama katika kata 14 ili kulinda usalama wa mtoto na kuhakikisha kila mtoto anapata elimu itakayomsaidia baadaye.

Mbali na hilo, wilaya hiyo imetekeleza agizo la serikali la kuunda majukwaa ya wanawake 13 ya kuelimisha jamii namna ya kuwalea watoto.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Denis Komba, alibainisha hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika katika Kata ya Zanka iliyoko Bahi.

Komba alisema lengo la kuanzisha kamati hizo ni pamoja na kuweka ulinzi wa mtoto kuhakikisha anakuwa salama dhidi ya ukatili wa kijinsia unaofanywa katika mazingira anayoishi na kusaidia kupata elimu.

Alisema kamati hizo zinafanya kazi ya kupambana na suala la ukatili ikiwamo kutoa elimu kwa jamii ya kujua umuhimu wa kumwachia mtoto akue salama ili atimize ndoto zake.

"Kamati hizi zinasaidia sana ulinzi na usalama wa mtoto, hutoa elimu kwa jamii lakini pia kuwachukulia hatua kali wanaobainika na vitendo hivyo," alisema Komba.

Alisema kumekuwa na matukio ya ukatili ambayo hufanywa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali, hivyo serikali imeunda kamati hizo kuhakikisha watoto wanakuwa salama dhidi ya ulatili wa kijinsia unaotendeka.

Komba alisema kamati hizo zimekuwa na msaada mkubwa wa kupunguza ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaobainika kufanya vitendo hivyo katika jamii inayotuzunguka.

Amos Mlungu kutoka Shirika la World Vision Tanzania mkoani Dodoma ambao ndiyo waandaaji wa maadhimisho hayo kwa kushirikiana na serikali na taasisi nyingine, alisema shirika hilo limekuwa likihamasisha kupinga masuala ya ukatili wa watoto ili waweze kukua katika malezi bora.

Alisema wameweka nguvu kuhamasisha jamii kwa kushirikiana na serikali kusaidia watoto yatima wanaoishi mtaani ili watimize ndoto zao za kielimu.

"World Vision Tanzania imekuwa ikitekeleza mikakati ua kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto kwa vitendo kwa kuandaa matukio mbalimbali ya kufundisha na kuielimisha jamii namna ya kumlinda mtoto ikiwamo kuwaongezea uelewa juu ya masuala ya mimba za ututoni pamoja na madhara ya mimba za ututoni," alisema.

Alisema shida kubwa wanayokutana nayo ni wazazi kutokutoa taarifa mapema pale watoto wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia.



# Mjini Magharibi Unguja kinara kudhalilisha watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKOA wa Mjini Magharibi Unguja umetajwa kuongoza kwa matukio mengi ya udhalilishaji watoto yakifikia 641 katika kipindi cha mwaka 2021.

Aidha Wilaya ya Magharibi 'A' inaongoza kwa kuwa na matukio 290 ikifuatiwa na Magharibi 'B' yenye mikasa 182 wakati wilaya ya Mjini yametajwa matukio 169.

Kwa mujibu wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, aliyeainisha hayo wakati akizungumza kwenye kongamano la maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika lililofanyika katika ukumbi wa Idrissa Abdul Wakil Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Alisema licha ya kuanzishwa Mahakama Maalum ya Kesi za Udhalilishaji na watuhumiwa wake kunyimwa dhamana, udhalilishaji wa watoto unazidi kuripotiwa.

Kadhalika, aliongeza kuwa serikali inakerwa na takwimu za matukio ya kesi za udhalilishaji zinazoripotiwa katika vituo vya sheria kwa sababu waathirika ni watoto.

Alisema takwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, mwaka 2021, jumla ya matukio 1,222 ya udhalilishaji yaliripotiwa wakati asilimia 12.6 waathirika ni watoto na Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ni kinara.

Aidha, alisema kati ya matukio hayo, 621 ni ya kubaka, 177 kulawiti, 83 kuingiliwa kinyume na maumbile, 95 kutorosha na 114 shambulio la aibu.

Alisema kwa mwaka 2022 mwezi wa Machi na April matukio 150 yameripotiwa na mkoa unaoongoza ni Mkoa wa Mjini Magharibi.

Aliongeza kuwa takwimu hizo hazifurahishi kwa sababu watoto wanaumizwa na kuhatarishiwa maisha yao, licha ya kwamba wanahitajika katika kuliongoza taifa.

Aliwataka wazazi kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa, wanatunzwa na kuendelezwa kielimu na kila hali.

Alisema bila kuwekeza nguvukazi nchi itakosa fursa ya kuendelea kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kukosa watu wenye utashi na utetezi wa taifa lao.

Aliwaambia washiriki kuwa makuzi ya mtoto yanahitaji matunzo na huduma tofauti ili akue kiafya, kimwili na kiakili.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Naibu Waziri wa wizara hiyo Anna Attanas Poul, aliwaasa watoto kujilinda na kutokubali kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Mjumbe wa bodi ya wadhamini wa Kijiji cha Kulela Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu (SOS), Rukiya Hamad Abdalla, alisema watoto wana haki ya kuadhimisha siku hiyo ambayo ni chachu ya malezi bora kwa mtoto na yanaamsha ari ya kumlinda zaidi.

Aliahidi kuwa SOS itaendelea kushirikiana na serikali kulea watoto vizuri, kuwapatia haki zao na kulidwa kwa nguvu zote.

Katika kongamano hilo mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo wajibu wa mtoto katika kukabiliana na udhalilishaji, jukumu la wazazi katika kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji, vyombo vya habari na viongozi wa dini katika kuzuia vitendo hivyo.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (aliyeshika kipaza sauti), akizungumza na Viongozi mbalimbali katika eneo linalojengwa maduka Darajani Mjini Unguja, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi ya ujenzi wa masoko mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamati Maalum ya CCM yaridhia Shamte kufukuzwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KAMATI Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Zanzibar imeridhia na kuunga mkono mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Mjini ya kumfukuza uanachama mwanasiasa mkongwe Baraka Shamte.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari Katibu wa Kamati Maalum, Idara ya Itikadi na Uenezi Zanzibar, Catherine Peter Nao, alisema kikao hicho kilichokaa wiki hii Juni 14, pamoja na mambo mengine kwa kauli moja kimeunga mkono pendekezo la kufukuzwa uanachama kada huyo.

Alieleza kwamba Baraka Shamte amegundulika kuwa na makosa makubwa ya itikadi yanayoathiri uhai wa CCM.

Catherine, alisema maamuzi hayo ya kuvuliwa uanachama yamezingatia ibara ya 13(d) ya katiba ya CCM ya 1977.

Aidha, kwa uzito wa kosa hilo kutokana na kifungu cha 12 fungu la tatu cha kanuni ya Usalama na Maadili za CCM, kwamba mtu anaweza kupewa adhabu yoyote kutokana na uzito wa kosa lake.

Katibu huyo alifafanua kuwa kikao hicho kwa kauli moja kimelaani kauli za uongo na uchochezi zilizotolewa na Baraka Shamte, dhidi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa Dk. Hussein Ali Mwinyi, alizozitoa kupitia mitandao ya kijamii.

"Kauli hizo, zimeleta uchonganishi mkubwa baina ya wananchi na serikali yao, vikao vya ngazi zote katika mfumo wa chama kwa ujumla."

Alisema kauli hizo hazina ukweli na zinapingana na katiba ya CCM ya mwaka 1977.

Aidha, zinapingana na ibara 15 (4) ya katiba ya chama, wajibu wa mwanachama kwamba,kuwa wakati wote ni mkweli,mwaminifu na raia mwema wa Tanzania, alifafanua Catherine.

Alisema kikao hicho, kimempongeza Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi anayoifanya ya kutekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025,kuhubiri amani, umoja, mshikamano na kuwaunganisha wananchi.

Pia, katibu huyo alisema kikao hicho kilipendekeza jina la aliyekuwa Naibu Katibu wa CCM Zanzibar, Vuai Ali Vuai, kuwa mmoja wa Wajumbe wa Baraza la Wadhamini wa CCM

## SMZ yataka ujenzi Jumbi na Mwanakwerekwe uanze tena

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, ameitaka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kuanza tena ujenzi wa masoko ya Jumbi na Mwanakwerekwe uliokwama.

Aidha, ameiagiza wizara hiyo kukaa na mwekezaji anayejenga masoko hayo na kufuata taratibu za kisheria ili kuendelea na ujenzi wa masoko hayo.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa miradi ya masoko hayo katika Mkoa wa Mjini Magharibi, alieleza kutoridhishwa na hatua iliyofikiwa ya ujenzi huo.

Alisema kuwa serikali itaangalia namna bora ya kujenga soko la Jumbi ili kuwasaidia wananchi na wajasiriamali kupata eneo zuri na la kisasa ambalo watajipatia huduma za kila siku.

Alisema serikali imeelekeza imani kwa sekta binafsi ili kushirikiana kupanua wigo wa ujenzi wa Zanzibar bora ambayo wananchi wake watafaidika.

Kadhalika, alimtaka mkandarasi wa soko la Mwanakwerekwe ambaye pia anaejenga soko la Jumbi kueleza changamoto zinazomkabili ili kufanyakazi kulingana na matakwa ya mkataba

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhamed, alisema wizara yake hairidhishwi kuona wawekezaji wanakwenda kinyume na makubaliano waliyofunga katika mkataba jambo linalochelewesha ujenzi wa miradi hiyo.

Waziri Mohamed, alieleza kuwa kwa kushirikiana na serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi hawatavumilia mwekezaji na mkandarasi atakayekiuka mikataba.

Katika ziara hiyo Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar alitembelea ujenzi wa soko la Darajani Bazaar na kueleza kuridhishwa kwake na hatua iliyofikiwa.

Katika ziara hiyo pia alitembelea Bandari ya Malindi na kujionea kazi ya kushusha na kupakia makontena na kuutaka uongozi wa Shirika la Bandari la Zanzibar kuweka mazingira ya kupunguza mrundikano wa makontena kwa kuyapeleka eneo la Bwanani ili kurahisisha na kufanyakazi kwa wakati.

Halikadalika alieleza kufurahishwa na maamuzi ya Shirika la Bandari kuweka One Stop Centre ya Shughuli za Bandari na kuwataka kuharakisha kukamilika kwa mfumo wa kuendesha kituo hicho ambapo kukamilika kkwake kutasaidia ukusanyaji wa mapato na kukuza uchumi wananchi.

"Kuwapo kwa 'one stop center' eneo la bandarini kutawapunguzia wafanyabiashara usumbufu wa kuhangaika kila sehemu kwa ajili ya kufanya malipo na kuwarahisishia wafanyakazi wa bandari kujua idadi ya kontena zinazoingia na zinazotoka pamoja na kudhibiti mianya ya rushwa," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**NEY UKIPENDA MWENYEWE ZITAKUTOKA**

Ukurasa.12





# Shilole umezidi

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Zuwena Mohamed, maarufu kama Shilole, amesema ameanza kufanya mazoezi ya kupunguza mwili ili kumfurahisha mume wake.

Hata hivyo, amewatahadharisha wanawake wanaomfuata fuata mume wake Rommy, kuacha mara moja kwa kuwa akigunduma atatoa kipigo kikali.

Shilole, ameeleza kwamba kwa sasa ana uzito wa kilo 107 na lengo lake ni kupunguza hadi kufikia 80. Amesema mazoezi aliyoyafanya kwa siku chache ameondoa kilo tatu jambo ambalo linamletea faraja kwamba anaweza kufikia malengo yake.

"Nataka kumfurahisha mume wangu, nimeanza mazoezi ya kupunguza uzito naamini nitafanikiwa muda sio mrefu," amesema Shilole.

Siku za hivi karibuni mwanamuziki huyo amekuwa akilalamikiwa na wafuasi wake kutokana na mwonekano wake wa unene kiasi ambacho kinapoteza uasilia wake.

Hata hivyo, amesema kitu kinachomnyima usingizi ni baadhi ya wanawake kumfuata mume wake, kwani katika ndoa ni jambo ambalo linamuumiza.

"Mimi sina maneno mengi nikigundua mwanamke anamfuata mume wangu natoa kipigo tu, jamani ndoa inauma na ndio maana unapoingia lazima uachane na mambo yote ya nyuma," amesisitiza.

BASI SAWA

## Tymilyfe, Apesi waibuka na 'Copy Pasting'



MSANII wa kizazi kipya kutoka nchini Kenya, Otieno Samson, maarufu kama Tymiliyfe, ameibuka kivingine na wimbo 'Copy Pasting' aliomshirikisha Apesi Mnyama Mkali.

Akizungumza na BT, Tymiliyfe amesema huo ni mwendelezo wa kutoa nyimbo kali ambazo zinaenda kumpa mashabiki wapya.

"Copy Pasting ni miongoni mwa nyimbo zangu kubwa, video na audio tayari nimevitoa na vipo kwenye chaneli yangu ya YouTube mashabiki wanaweza kwenda kuicheki na kupata ladha tofauti ya muziki," amesema Tymiliyfe msanii ambaye anaishi Uingereza.

## Milyon azidi kuwapelekea 'moto'



MSANII wa kizazi kipya, George Nashon, maarufu kama Milyon, amewaomba wapenzi wa muziki kuipokea video ya wimbo wake mpya unaoitwa Moto.

Milyon, ameliambia BT kuwa amekuwa kimya kwa muda mrefu kutokana na kujipanga upya, sasa amerudi akiwa na ngoma hiyo ambayo tayari inasumbua kitaa.

"Sasa ni mwendo wa kuwapa burudani mashabiki, nimeachia Moto na tayari nimeona mapokezi yamekuwa makubwa tofauti na nilivyotarajia japo bado nahitaji kuona mashabiki wakinipa sapoti zaidi," amesema Milyon.



## Starshine awakomesha kwenye amapiano

MSANII anayekuja kwa kasi kwenye Bongo Fleva, Starshine, ametamba kuwa wimbo wake 'Ananivuruga' ndio muziki bora katika mtindo wa amapiano.

Akizungumza na BT jana, Starshine, amesema zipo amapiano za mastaa wengi kama Diamond Platnumz, Harmonize lakini wimbo wake ndio bora kwasasa akiwa ndani yake amemshirikisha Fatma Fettyslay.

"Ananivuruga ni moja ya amapiano bora zaidi, ni kali ukilinganisha na amapiano zilizotoka 2022, mtu yeyote akisikiliza atakubaliana na mimi, video ipo kwenye channel yangu ya YouTube kila mmoja anaweza kuisikiliza," amesema Starshine a.k.a mtoto wa mama Danny.



## Ney ukipenda mwenyewe zitakutoka

RAPA mwenye utata, Ney wa Mitego, amesema tangia aanze mapenzi hajawahi kuhonga mwanamke, na kamwe hatafanya hivyo katika maisha yake.

Amesema yeye ana tabia ya ubahili kwa asilimia 100, kutokana na asili ya wazazi wake ambao ni mchaga na mnyakyusa.

"Mimi huwa namuhudumia mwanamke ninayempenda, sina tabia ya kuhonga kama wanavyofanya wengine," amesema Ney wa Mitego.

## Wanamuziki wanasifia wake zao

**Na Adam Fungamwango**

MARA nyingi duniani mtu hukisifu kilicho chake na ni vizuri kukisifu unachokipenda. Sijajua kama wasanii wa muziki wa kizazi kipya kwenye nyimbo zao ambazo asilimia 90 za zaidi zimelenga kwenye mapenzi kama kuna yoyote ambaye amemtungia mpenzi wake wa kweli au mkewe, huku akimtaja jina kwenye wimbo.

Sitaki kuingia kwa undani kujua ambao huwa wanawaimba ni akina nani, lakini wanamuziki wa dansi wa zamani pamoja na asilimia kubwa kutunga nyimbo zenye matukio ya kweli, lakini pia walikuwa wanatunga nyimbo za kuwasifu wapenzi au wake zao.

Na walikuwa hawafichi, hivyo hata mashabiki wao walikuwa wanajua kabisa kuwa wimbo huu mtunzi au mwimbaji fulani amemuimba mkewe.

**ASHA MWANASEFU-TX MOSHI WILLIAM**

Ndiye mwanamuziki anayeongoza kwa kumtungia mkewe nyimbo nyingi kuliko mwingine yoyote. Alimtungia nyimbo tatu.

Tx Moshi William aliyefariki mwaka 2006 akiwa na bendi ya Msondo Ngoma Music, wakati anaingia tu kwenye bendi hiyo mwaka 1982, ikiitwa Juwata Jazz, alimtungia mkewe Asha Sefu wimbo unaitwa 'Hamida'. Hilo pia ni jina la mkewe huyo huyo. Baadaye akatunga wimbo unaitwa 'Asha Mwanasefu', jina ambalo ni maarufu zaidi na hata wimbo huo ukawa maarufu zaidi kuliko nyingine alizomtungia.

Wimbo mwingine aliomtungia mkewe huyo huyo unaitwa 'Cheusi Magala' Magala ni jina pia la kiasili la mkewe huyo huyo, Asha.

**LUCY BANDAWE-ATHUMANI MOMBA**

Huyu ni mwanamuziki aliyepitia bendi nyingi kama vile Dar International, Vijana Jazz, Bima Lee na Msondo Ngoma Music.

Akiwa na Msondo alimtungia mkewe wimbo uitwao 'Lucy Bandawe'. 'Lucy Bandawe nipeleke Nyasa...' ni moja kati mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo aliyomtungia mkewe. Lucy ni mwanamichezo wa zamani, kwani alikuwa mashuhuri kwenye mchezo wa netiboli alizichezea klabu mbalimbali za zamani.

Momba mwimbaji wa sauti kali ya kwanza kiasi cha kubatizwa jina 'sauti ya chuma', alifariki dunia 2005.

**ZARINA-HASSAN BITCHUKA**

Ni wimbo wa 'Zarina' ulipigwa katikati ya miaka ya 1970. Ni kipindi ambacho bendi hiyo inatoka kuitwa Nuta jazz na kuwa Juwata Jazz wana Msondo Ngoma.

Kwa mujibu wake mwenyewe anasema alimtungia na kumuimbia mkewe, hivyo naye anaingia kwenye kundi la wanamuziki waliowatungia nyimbo wake zao.

**MAMA FERI-COSMAS CHIDUMULE**

Mwanamuziki huyu wa zamani wa bendi za Butiama, Western, Kurugenzi, akiwa na bendi ya DDC Mlimani Park aliwa hukutunga wimbo unaitwa 'Mama Feri'. Huu alimtungia mkewe Cecilia Michael wakati huo miaka ya 1980.

"Kumbe hata kwa ndugu zako umefikisha malalamiko yako, eti nina mpango wa kuoa mke mwingine, badala yako, wazo hilo sina mama..." Yalikuwa ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo. Chudumule kwa sasa ameachana na nyimbo za kidunia na kujikita kwenye nyimbo za Injili.

**TULELE TUBOE-MIKIDADI SEIF**

Alikuwa ni mwanamuziki wa bendi ya Uda Jazz ambaye alifariki hivi karibuni mkoani Lindi. Mikidadi kwenye miaka ya 1980 alitunga wimbo wa 'Tulele Tuboe'. Alimtungia aliyekuwa mkewe Suzana Makota kuwa waishi walee watoto. Wimbo huo aliutunga na kuimba kwa lugha ya Kimwera.



TX MOSHI WILLIAM



## Barua ya Jini; Mapenzi hayana ulinganifu

**Na Adam Fungamwango**

NI filamu inayohusu vita kali ya kugombea mapenzi kati ya binadamu na jini inaitwa 'Barua ya Jini' ambayo imechezwa na waigizaji kina Ally Kizo aliyecheza kama Songoro, Jenifa Michael yeye ni Lina, Rachel Maulidi kama dada yake Songoro, Hanifa Said akicheza kama Asha, na wengineo walishiriki.

Majini ni moja kati ya viumbe vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu, lakini vikiwa na uwezo wa kujibadilisha kwa muonekano wowote ule wanaoupenda.

Songoro na Lina ni wapenzi wanaopendana sana kiasi cha kutaka kuoana. Hata hivyo kuna siku Songoro anaopoa demu mmoja kwa namna ambayo hata yeye hajui amekubali vipi.

Baada ya siku chache anaokota bahasha, lakini ikiwa na ujumbe na pesa. Hata hivyo ujumbe huo ulioandikwa haueleweki vizuri anatokewa na mtu ghafla.

Mtu yule anamkumbuka kuwa ni yule demu. Akajitambulisha kwa jina la Asha na kumwambia yeye hakuwa binadamu wa kawaida bali ni jini.

Akamwambia alimpa mapenzi ya ajabu siku walivyokutana kiasi anaomba awe wake peke yake na asiwe na mtu yoyote.

Kali kuliko yote akamkataza Songoro kuwa na uhusiano tena na Lina. Akamwambia kwa sababu yeye ni jini anaweza kujibadilisha na kuwa kama Lina au mwanamke yoyote yule mrembo duniani hata Beyonce, hivyo akitaka atakuwa anajibadilisha kuwa kama Lina.

Hiyo inamfanya Songoro kuwa na mawazo sana. Jini Asha anamtokea Lina na kumwambia aachane na mpenzi wake Songoro kwa sababu yeye anampenda sana.

Lina anafanya ubishi. Bado anakwenda kwa mpenzi wake Songoro. Kinachofanyika ni kwamba jini Asha anamgeuza Lina kuwa kipofu kwa dakika tano na baadaye anamfanya kuona. Anamwambia hilo ni onyo, akirudia atamfanya kuwa kipofu daima. Lina akawa na woga, akawa haendi kwa Songoro.

Jini Asha na Lina wote sasa wakawa wajawazito. Mama yake Lina akaja kumwambia Songoro ni lazima amuoe binti yake kwa sababu ameshampa ujauzito. Jini Asha anamtokea Songoro na kuwambia ana mimba yake. Na ili awe salama kwa majini wenzake na wazazi wake ni lazima waoane. Songoro anakataa.

Kwa hasira Asha anamgeuza taahira ambaye anashinda na kulala chini ya mti. Kila siku Asha anakuja na kumbembeleza waoane, pia akimtahadharisha kuwa kama akikataa, ataishi hivyo milele.

# Bierber anaamini Yesu yupo



MWANAMUZIKI nyota wa Pop nchini Marekani, Justin Bierber, amesema anaamini tatizo la kupooza uso linalomkabili litapita kwa kuwa anamwamini Yesu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Bierber mwenye miaka 28, amesema ugonjwa huo unaojulikana kama ramsay Hunt Syndrome, ni sawa na dhoruba na itafikia muda litapita.

"Ninafahamu dhoruba hii itapita lakini wakati huo huo Yesu yuko nami ," Bieber aliandika.

Ugonjwa huo hutokea wakati vimelea wanaposhambulia neva za uso karibu na masikio ya mtu.



## Burna Boy bado hujatulia tu

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria Burna Boy, na washirika wake wameshutumiwa kwa kujeruhi wafuasi wake katika klabu moja ya usiku.

Wiki iliyopita, baadhi ya watu walijitokeza na kudai walishuhudia jinsi msanii huyo na rafiki zake walivyowafyatulia risasi baadhi ya watu waliokuwa wakiburudika katika klabu moja maarufu mjini Lagos.

Katika tukio watu kadhaa waliopigwa risasi wamejitokeza kueleza kisa hicho.

## Bakassi utani mwingine haufai

MCHEKESHAJI na mwigizaji kutoka Nigeria, Okewy Bakassi, amempa changamoto mgombea urais Peter Obi, baada ya kueleza anafanya ziara ya Misri.

Msanii huyo mkongwe, ametumia ukurasa wake wa Twitter, amesema ni jambo la kushangaza kuona mgombea wa ngazi ya juu anakwenda nchi za nje na kuacha kampeni.

"Peter Obi ametupa hasira kwani anakwenda Misri kwa ajili ya biashara na kisha London kufanya uchunguzi wa afya yake," ameandika msanii huyo.





## Ada pole, Mungu atakusaidia

MWIGIZAJI wa kike kutoka Nollywood, Ada Ameh amefichua kwamba anaelekea kupata matatizo ya kiakili na kuathiri afya yake.

Katika ujumbe wake kupitia ukurasa wa Instagram, Ada amesema hawezi kufanya majukumu yake ya kikazi kutokana na kukabiliwa na tatizo hilo.

"Kila kitu kinakwenda vizuri sasa ninapozungumzia maisha yangu, nina jambo naweza kufa kwani nilipata kazi lakini nikashindwa kufanya kutokana na kukabiliwa na tatizo la kiakili," amesema.

## Moses ona sasa umejichumia janga

MSANII mkongwe wa filamu kutoka Nigeria, Moses Armstrong, amekamatwa na polisi baada ya kutuhumiwa kumbaka binti wa miaka 16.

Kulingana na taarifa mbalimbali, mwigizaji huo amekamatwa na polisi wa jimbo la Akwa Ibom, kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka ya kosa hilo.

Rais wa wasanii wa filamu nchini humo, Emeka Rollas, amesema suala hilo linashughulikiwa katika umakini na serikali imelichukulia katika hali tofauti kutokana na msichana huyo kuwa na umri wa chini ya miaka 18.



MAKALA

# Utafiti unaposhindwa kubaini chanzo cha binadamu kulala muda mfupi

Mwandishi Wetu



MUDA wa kulala kwa binadamu umekuwa mchache ukilinganisha na wanyama wengine kama nyani na Sokwe.

Katika usiku wa kiangazi, wawindaji wa kabila la San nchini Namibia, mara nyingi hulala chini ya mawe wakiangaziwa na nyota. Hawana taa za umeme au ili kuwafanya wawe macho.

Hata hivyo, wanapoamka asubuhi huwa hawajalala kwa muda mwingi, lakini wenzao wa majiji makubwa ya Marekani na Ulaya wamekuwa macho wakitazama simu zao.

Kulingana na mwanaanthropolojia wa mageuzi, David Samson kutoka Chuo Kikuu cha Toronto cha Mississauga, utafiti mpya umeonyesha kuwa watu katika jamii zisizo za viwanda ambazo hukaribia sana na mazingira ambayo spishi zetu ziliibuka, hulala chini ya masaa saba kwa usiku.

Utafiti huo wa kushangaza unaonyesha wanyama wanaokaribiana na binadamu wanalala kwa muda mrefu zaidi.

Sokwe hulala takribani saa 9.5 kwa siku moja na nyani wenye vichwa vyeupe hulala kwa saa 13.

Samson anaita tofauti hizo ni kama kitendawili cha usingizi wa mwanadamu.

"Inawezekanaje sisi ni nyani ambao hulala muda kidogo?" anahoji.

Usingizi unajulikana kuwa muhimu kwa kuboresha kumbukumbu, kinga ya mwili, na mambo mengine ya afya zetu.

Mamilioni ya miaka iliyopita, babu zetu waliishi, na labda walilala kwenye miti. Hata leo, sokwe na nyani wengine hulala kwenye vitanda au maeneo ya muda kwenye miti. Wanapinda au kuvunja matawi ili kuunda umbo la bakuli, ambalo wanaweza kutandika matawi ya majani wakati mwingine hujenga vitanda chini.

Wazee wetu walitoka kwenye miti ili kuishi chini na wakati fulani walianza kulala huko pia. Hii inamaanisha walilazimika kuacha faida zote za kulala kwenye miti, pamoja na usalama kutoka kwa wanyama wanaowinda kama vile simba.

Mabaki ya mababu zetu hayaonyeshi jinsi walivyokuwa wamepumzika. Ili kujua jinsi gani binadamu wa kale walivyokuwa wakilala, wanaanthropolojia wametafuta ushahidi kutokana na jamii za kisasa zinazoishi porini.

"Ni heshima kubwa na nafasi kubwa kufanya kazi na jamii hizi," anasema Samson, ambaye amefanya kazi na wawindaji wa Hadzabe nchini Tanzania, pamoja na vikundi mbalimbali nchini Madagascar na Guatemala.

Ili kuweka pamoja historia ya mabadiliko ya usingizi wa mwanadamu, David Samson aliweka kile anachokiita dhana yake ya usingizi wa kijamii ya Anthropolojia ya mwaka 2021.

Kulingana na Samson, usingizi mfupi na wenye kunyumbulika huenda uliibuka kutokana na tishio la uwindaji wakati wanadamu walipoanza kulala chini.

Anadhani sababu nyingine ya kulala salama ardhini ilikuwa ni kulala kwenye kundi.

"Tunapaswa kuzingatia kambi za kwanza za binadamu na vikundi kama ganda la konokono," anaeleza.

Vikundi vya wanadamu viliweza kushiriki makazi rahisi. Moto ulitumika kuwalinda kwa kuwazuia wadudu na kuwapa joto nyakati za usiku.Baadhi waliweza kulala huku wengine wakisimama kuwalinda.

Kulingana na Isabella Capellini, mwanaikolojia wa Chuo Kikuu cha Malkia huko Belfast, Ireland Kaskazini, anasema ni jambo linaloweza kukubalika kwamba tishio la wanyama wanaowinda wanyama wengine lilifanya binadamu wapate usingizi kidogo kuliko nyani wanaoishi kwenye miti.

Katika utafiti wa 2008, yeye na wenzake waligundua kuwa mamalia walio katika hatari kubwa ya kuwindwa walilala kidogo na kwa wastani.

Lakini Capellini hana uhakika kwamba usingizi wa binadamu ni tofauti na ule wa nyani wengine kama inavyoonekana.

Anasema kwamba data iliyopo juu ya usingizi wa nyani inatoka kwa wanyama wanaofungwa na sio wale walio kwenye mazingira yao halisi.

"Bado hatujui mengi kuhusu jinsi wanyama hulala porini," anasema.

Katika zoo au maabara, wanyama wanaweza kulala chini ya kawaida, kutokana na matatizo. Au wanaweza kulala zaidi.

"kwa sababu tu wanyama hulala sana wakiwa wamechoka" anasisitiza Capellin.

Katika utafiti wa 2008, Rattenborg na wenzake walifunga mashine za elektroniki kwa wanyama wanaofanana na binadamu wa porini na wakagundua kuwa wanyama hao walilala karibu saa 9.5 kwa siku. Utafiti wa awali wa wanyama hao ulirekodi karibu saa 16 za kulala kwa siku.

Kuwepo kwa data zaidi kutoka kwa wanyama pori kungesaidia watafiti wa usingizi kugundua ukweli.

"Lakini kiufundi ni vigumu kupata," anaongeza kusema Rattenborg.

Ikiwa wanasayansi wangekuwa na picha ya wazi ya kulala kwa nyani porini, inaweza kuibuka kuwa usingizi kwa binadamu sio mfupi sana kama inavyoonekana.

> **Ni heshima kubwa na nafasi kubwa kufanya kazi na jamii hizi," anasema Samson, ambaye amefanya kazi na wawindaji wa Hadzabe nchini Tanzania, pamoja na vikundi mbalimbali nchini Madagascar na Guatemala**

Yetish, ambaye anachunguza usingizi katika jamii ndogo ndogo, ameshirikiana na Samson katika utafiti.

Yetish anaelezea jioni ya kawaida kati watu wa Tsimane: baada ya kutumia siku kufanya kazi mbalimbali, kikundi hukusanyika karibu na moto wakati chakula kinapikwa. Wanashiriki chakula, kisha wanakaa karibu na moto gizani.

Watoto na akina mama polepole husogea kwenda kulala, wakati wengine hukaa macho, wakizungumza na kusimulia hadithi.

Hii ndiyo sababu Yetish anapendekeza kwamba wanadamu wa kale walilala saa chache kwa kubadilishana habari na utamaduni kando ya moto.

Huenda babu zetu walipunguza usingizi wao kwa muda mfupi kwa sababu walikuwa na mambo muhimu zaidi ya kufanya usiku kuliko kupumzika.

Swali la ni kiasi gani tunalala ni tofauti na swali la kiasi gani tungependa kulala.

Samson na wengine waliwauliza washiriki wa somo la Hadzabe jinsi walivyohisi kuhusu usingizi wao wenyewe. Kati ya watu 37, 35 walisema walilala vya kutosha", timu hiyo iliripoti hilo

Kiwango cha wastani walicholala katika utafiti huu kilikuwa kama saa 6.25 kwa usiku. Lakini waliamka mara kwa mara, wakihitaji zaidi ya saa 9 kitandani kupata hizo saa 6.25 za usingizi.

Kinyume chake, uchunguzi wa 2016 wa karibu watu 500 huko Chicago uligundua kuwa walitumia karibu muda wao wote kitandani kulala na walilala kama jamii ya Wahadzabe.

Bado karibu asilimia 87 ya waliohojiwa katika uchunguzi wa 2020, watu wazima wa Marekani walisema kwamba angalau siku moja kwa wiki hawakuhisi kulala.

Kulingana na Samson, ufahamu bora zaidi wa mabadiliko ya usingizi kwa binadamu unaweza kuwasaidia watu kupumzika vizuri.

"Watu wengi Kaskazini na Magharibi wanapenda kulalamikia kukosa usingizi au usingizi wao kuwa mchache," anasema.

BBC

MAKALA

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko vya madenti zamani kupenda barua za kikubwa

## •Waliobambwa wasimulia cha moto

Na Adam Fungamwango



MAISHA yanaenda kasi sana. Siku hizi watu wanatumiana meseji kwenye simu za mkononi na hata mitandao ya kijamii, ikiwemo email, WhatsApp, facebook, instagram na mingine mingi kwa mawasiliano.

Hata wapenzi wa sasa wanatumia ili kurahisisha mawasiliano tofauti na zamani ambapo ilikuwa ni ngumu sana.

Wakati huo watu walikuwa wakikutana wanaahidiana tu kuwa watakutana sehemu fulani, siku fulani na saa fulani.

Sasa kama siku hiyo mmoja, kaamka hajisikii vizuri, au mzazi wake amemkataza kwenda popote, aliyebaki ni lazima atafika tu sehemu hiyo na kukaa muda mrefu bila kujua nini kimempata mwenzake. Na hiyo ni mpaka tena wakutane ndiyo atakapomwambia kuwa siku ile kulikuwa na tatizo fulani.

Siku hizi unaamka, mpenzi anamtumia mwenzake meseji "shangazi anaumwa leo siwezi kuja hadi Jumapili."

Hiyo inasaidia kuwa huwezi tena kwenda kwa sababu taarifa imeshatoka kuwa imeshindikana.

Wadau leo wameomba niweke mada ya baadhi ya wanafunzi ambao walipata bahati mbaya kwa kukamatwa wakiwa na barua za mapenzi shuleni enzi hizo.

Wakati naiandaa, wanafunzi wa zamani waliopatwa na dhahama hiyo walieleza hisia zao na kukumbuka jinsi walivyokamatwa na barua hizo na hatua walizochukuliwa na walimu.

Jinsi walivyoelezea inafurahisha sana na kukumbusha jinsi wanafunzi zamani walivyokuwa watundu mno.

Kwanza kabisa ni lazima ieleweke kuwa enzi hizo wanafunzi wengi walikuwa wakianza shule darasa la kwanza wakiwa wakubwa. Si miaka mitano au saba kama ilivyo sasa.

Siku hizi wanafunzi wanaanza chekechea wakiwa wadogo na hata shule za msingi na kumaliza wakiwa wadogo sana tofauti na zamani.

Enzi hizo mwanafunzi wa darasa la saba anakuwa 'baba zima' au kama msichana kama asingekuwa anasoma shule basi angekuwa ameolewa.

Wavulana kwa wasichana walikuwa wakianza shule miaka 10, au na kidogo kwenda juu, hivyo wakiwa shule ya msingi tu wanakuwa wamepevuka.

Hii wakati mwingine iliwaletea matatizo sana hasa wanafunzi wa kiume, kiasi cha kuanza kuandika barua za mapenzi kwa wanafunzi wasichana kitu ambacho ni marufuku kabisa, kwani ikibainika basi adhabu yake ya juu kabisa ni kutimuliwa shule.

Kabla hawajafunguka wanafunzi wa zamani ni kwamba kulikuwa na uandikaji barua za mapenzi. Ulikuwa ni kama utaratibu hivi. Usipoandika au kufanya hivyo unaonekana kujui kuandika barua ya mapenzi, iwe shuleni au mitaani.

Kwanza itaanza na neno "njiwa peleka salamu kwa yule nimpendaye." Halafu baada ya hapo itaendelea na "Pokea salaam nyingi sana zisizo na kifani toka moyoni mwangu la Aziz, natumai u buheri wa afya, baada ya salaam mimi sijambo. Madhumuni ya barua hii ni kukujulisha kuwa nakupenda sana...mwenzio sipati hata lepe la usingizi kila ninapokuwaza, usiku kucha silali nakuota wewe..."

Hapo zitaendelea mbwembwe nyingi na sanaa za uandishi wa kila mmoja na mwishoni barua hiyo itaishia hivi. "Nashukuru kama utanikubalia ombi langu. Wako akupendaye kwa dhati."

Wanafunzi wa zamani wakaibuka kuanza kutuma visa vyao kwenye mtandao wangu wa kijamii na simu.

Kama kawaida, wengi wao huwa hawapendi majina yao kuchapishwa kwa sababu kwa sasa ni watu wazima, wenye familia zao, lakini baadhi wana nyadhifa mbalimbali serikalini na maeneo mengine ya ujenzi wa taifa.

Mmoja alinitumia meseji akaniambia.

"Dah, nilishawahi kuandika barua kwa msichana mmoja shule ya msingi, kabla ya kumkabidhi mlengwa nikaiweka katikati ya daftari. Nikajisahau madaftari yakakusanywa kwa mwalimu wa darasa, akaiona. We bwana wee, nilikula bakora si za kawaida." Anasema denti huyo wa zamani.

Mwingine aliyeniandikia ni mama, wakati huo ni msichana tu mwanafunzi wa shule ya msingi.

"Mimi niliandikiwa barua na mvulana mmoja mwanafunzi mwenzangu mimi sijui, akamtuma rafiki yangu aje kuniomba daftari. Sikujua kitu kumbe lile daftari ni kwa ajili ya kumpelekea huyo mvulana aiweke barua kwenye kurasa za daftari langu, kumbe ile picha mwalimu darasani aliiona. Akachukua daftari, akaiona barua ile, ikagongwa kengele, ikasombwa msitarini, tulikula bakora za kutosha, mimi, rafiki yangu na huyo mvulana. Ila mimi jamani walinionea, sikuwa najua lolote." Alifunguka mama huyo ambaye kwa sasa anasema ana wajukuu.

Mwingine huyu yeye alilifanya jambo hilo kwake kuwa fursa, na yeye pia akifukuzia demu.

"Kuna jamaa mmoja alikuwa hajui kusoma, halafu ni mtoto wa mwalimu, tulikuwa darasa la tano, akawa amempenda msichana mmoja anaitwa Mariam, ambaye pia mimi nilimpenda.

Basi akawa ananiomba nimsaidie kuandika barua ya kumpelekea Mariam kwa kuwa anampenda na kuahidi kunilipa kwa kazi hiyo.

Nikakubali kwa kuwa nilitaka pesa na msichana pia, sasa nilichokuwa nafanya nikawa naandika barua ambayo mimi ndiyo natongoza. Nikimaliza namsomea vilevile ilivyo, lakini nikiweka kuwa yeye ndiyo mhusika, akawa anafurahi na kunipa pesa. Na yeye mwenyewe ndiye aliyekuwa anapeleka kwa sababu ndiye mwenye barua, lakini kwa sababu nimeandika mimi nikawa naweka jina langu. Demu alikubali, lakini kabla ya chochote hakijafanyika, jamaa anaona mbona msichana hamchangamkii kama kweli amekubali, akashtuka kuwa nimemzunguka, ukaanza ugomvi, alinipiga kwa kuwa yeye alikuwa mkubwa kuliko mimi na ilisababisha jambo hilo kujulikana shule nzima na walimu, adhabu ikatembea." Anasema mhusika mwingine.

Mchangiaji mwingine yeye aliniandikia "wakati nipo darasa la nne kulikuwa na msichana mmoja mwanafunzi nampenda sana, lakini nilikuwa naogopa kumwambia, nikamuandikia barua, lakini kabla ya kumpa nikaipoteza, kumbe rafiki zangu waliiokota na kumpelekea mhusika, akaiwasilisha kwa mwalimu ikawa balaa kubwa."

Sasa kuna huyu aliyekamatwa na barua akaanza kuzitafuna, akaniandikia.

"Tulipigwa sachi ya maana darasani wote wenye tabia ya kuandika barua za mapenzi, mwalimu na viranja wanafanya kazi hiyo, mimi nilikuwa nayo moja, nikaitafuna, wakaniona. Wakaanza kusachi madaftari yangu, wakaikuta nyingine ambayo ndiyo iliyohaririwa kutokana na maneno ya barua ya kwanza niliyoitafuna. Ikasomwa, nikapata mkong'oto wa haja, huku mwalimu ambaye alikuwa mwanamke akiniuliza wewe maneno haya ya kikubwa umeyatolea wapi? Yule msichana niliyemwandikia alikuwa anacheka tu. Bahati nzuri tulikutana tena ukubwani, tulipoonana kila mmoja alianza kucheka." Anasema mdau huyo.

Tumalizie na mchangiaji huyu ambaye yeye alitoa kali kwa kumuandikia barua ya mapenzi mwalimu wake.

"Wakati nipo darasa la sita, kuna mwalimu mpya wa kike alihamia pale shuleni kwetu kwa ajili ya kutufundisha somo la sayansi. Alikuwa mweupe, bado binti tu. Wanafunzi tulikuwa tunampenda sana maana hakuwa mkali sana.

Siku moja tupo class nikawaambia jamaa zangu wawili niliokuwa nakaa nao kwenye dawati moja, kuwa nitamuandikia barua yule ticha, halafu kama masihara niliiandika kweli ile barua japo sikuwa na dhamira ya kumpelekea. Nikaiweka kwenye mfuko wa nyuma wa kaptura ya shule nikaisahau.

Kesho yake yule ticha baada ya kumaliza kipindi chake, akawa karudi ofisini, akasahau chaki zake darasani, akaniagiza nimchukulie chaki zake nilete ofisini.

Nilimbebea chaki zake nikaziweka kwenye mfuko wa kaptura, kumbe wakati nazitoa nimpe, ile barua ikaanguka, ila sikujua. Inavyoonekana ticha aliiokota na kuisoma." Jamaa hakuishia hapo, akaendelea.

"Nikawa nashangaa tokea siku hiyo kila akiniona anacheka tu, na akija darasani lazima niulizwe maswali muda wa kipindi chake, mara utaskia akisema 'we mtu mzima njoo ufute ubao.' Akaanza kufatilia maendeleo yangu kama vile mtu tunayefahamiana.

Kuna siku baada ya kipindi chake akaniambia nimbebee madaftari tuliyokusanya darasani, tulipofika ofisini akaniambia 'dogo soma kwanza, mapenzi hayatokufikisha popote.' Nikaanza kujiuliza maswali, hapo hapo nikaikumbuka barua yangu ambayo siioni kwenye kaptura, nikajua ameibamba na kuisoma, lakini wala hakuniambia wala kumwambia mtu yoyote yule." Anasema baba huyu ambaye wakati huo alikuwa denti tu.

Anasema baada ya miaka zaidi ya 20 akiwa amemaliza shule katika purukushani za maisha akakutana naye.

"Uzuri mimi ndiyo nilikuwa wa kwanza kumuona na kumtambua, nikataka kumkimbia kumbe alikuwa ameniona na ilikuwa kwenye kituo cha basi na asingeweza kunisahau kwa sababu tulijenga ukaribu kuanzia darasa la sita hadi sasa, hasa baada ya ile barua bila mimi mwenyewe kujua. Mara nikasikia sauti 'dogo upo kwenye kusaka pesa au bado unaendekeza mapenzi?. Halafu mbona unanikwepa, au hutaki jibu la barua yako?' yaani we acha tu nimekumbuka mbali sana."

**Tuma meseji 0716 350534**

# Ulaya yapendekeza Ukraine kuwa mwanachama kamili

**BRUSSELS,** UBELGIJI

KAMISHENI ya Ulaya imependekeza nchi ya Ukraine iruhusiwe kujiunga uwanachama wa Umoja huo.

Wakati ombi hilo limekubaliwa, mashambulizi makali yanaendelea kufanywa na vikosi vya Russia mashariki mwa nchi hiyo kwa dhamira ya kutwaa udhibiti kamili wa jimbo la Donbas.

Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, ndicho chombo cha utendaji cha umoja huo, ambayo ilikutana mjini Brussels nchini Ubelgiji kuridhia ombi la Ukraine lilotolewa siku nne tu baada ya Russia kuanza kuivamia.

Nchi nyingine mbili zilizokuwa kwenye Muungano wa Kisovieti, Georgia na Moldova, nazo zilituma maombi kama hayo.

Kama ilivyo kwa Ukraine, mataifa hayo nayo yanakabiliwa na makundi ya wanaotaka kujitenga kwenye mikoa inayokaliwa na vikosi vya Russia.

Kikao cha jana kilitanguliwa na ziara ya viongozi wa mataifa matatu makubwa ndani ya Umoja wa Ulaya iliyofanywa nchini Ukraine ambayo ililenga kuonyesha mshikamano wao.

**VIONGOZI WA ULAYA WAIUNGA MKONO UKRAINE**

Viongozi wa Ufaransa, Ujerumani na Italia walimuelezea Rais Volodymyr Zelensky, uungaji wao mkono kuhusu kujiunga na jumuiya hiyo.

Kansela Olaf Sholz wa Ujerumani, alisema baada ya mazungumzo yao na Zelensky kwamba Ukraine ni sehemu ya familia ya Ulaya.

Ukraine, Moldova na Georgia zitakabiliwa na mchakato mrefu wa kutimiza vigezo vinavyotakiwa ili kupata uwanachama kamili, na huku kukiwa na wagombea wengine wanaosubiri kupatiwa uwanachama huo.

Vile vile, hatua hiyo haimaanishi kuwa ni uhakika wa kupatiwa uwanachama, ikizingatiwa mfano wa Uturuki, ambayo imekuwa mgombea uwanachama tangu mwaka 1999.

**MASHARIKI MWA UKRAINE KWAZIDI KUSHAMBULIWA**

Gavana wa jimbo la Luhansk, Serhiy Haidai, alisema jana kiwanda kikubwa cha kemikali cha Azot kimebomolewa kabisa na makombora ya Russia.

Kuna wasiwasi mkubwa juu ya hatima ya raia waliokuwa wamejificha kwenye majengo ya kiwanda hicho.

Kupitia mtandao wa Telegram, Gavana Haidai alindika: Hakuna tena jengo lolote lisiloharibiwa kwenye eneo lote la kiwanda hicho cha kemikali.

Hata hivyo, gavana huyo aliongeza kwamba bado vikosi vya Ukraine vinaonyesha upinzani mkali dhidi ya wanajeshi wa Russia ambao wamekuwa wakilishambulia eneo hilo kwa wiki kadhaa sasa.

**UFARANSA YAKATIWA MGAO WA GESI KUTOKA UJERUMANI**

Shirika la bomba la gesi nchini Ufaransa, GRT gaz, limesema ugavi wa nishati hiyo inayoingia Ufaransa kutokea Ujerumani umesitishwa tangu jana.

Taarifa hiyo ilisema hali hiyo inatokana na athari za kupungua kwa mgao wa gesi kutoka Russia.

Waratibu wa gridi ya nishati hiyo nchini Ufaransa wamechapisha tangazo, wakiwataka waagizaji kujaza maghala ya gesi ya taifa kadri wawezavyo wakijiandaa kwa majira yajayo ya baridi.

Waratibu hao hata hivyo walisema Ufaransa haitakabiliwa na tishio la kukosa gesi, kwa sababu nakisi katika mgao utokao Ujerumani inafidiwa na nishati inayoingia kutoka Uhispania. Walisema hivi sasa akiba ya kimkakati ya nchi hiyo iko katika kiwango cha asilimia 56, ambacho ni cha juu ikilinganishwa na asilimia 50 ambayo ni ya kawaida katika kipindi cha mwaka.

**DW**

# Waasi wa M23 waliazimia kuukamata mji wa Goma

**GOMA,** DRC

WATAALAMU huru wa Umoja wa Mataifa kuhusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, wamesema kuwa waasi wa M23 walipanga kuukamata mji wa Goma ili kuishinikiza serikali kuridhia matakwa yao ya kisiasa.

Mapigano ya hivi karibuni kati ya waasi hao na vikosi vya serikali ya Congo yaliibua mvutano mkubwa wa kikanda, huku DRC ikiituhumu Rwanda kuwaunga mkono waasi hao.

Hata hivyo, Rwanda imekanusha kuwasaidia waasi wa M23 ambao wiki hii waliukamata mji wa kimkakati wa Bunagana ulio mpakani na Uganda.

Ripoti ya wataalamu wa Umoja wa Mataifa iliyoandikwa Juni 14, ilieleza malengo ya waasi hao ni kuuzingira mji wa Goma, ili baadaye waweze kuukamata.

Mji wa Goma wenye wakaazi wapatao milioni moja, ni makao makuu ya mkoa wa Kivu Kaskazini, na ni kituo kikuu cha biashara kwenye mpaka kati ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo **DW**

# Korea Kaskazini yakumbwa na ugonjwa wa tumbo

**PYONG YANG,** KOREA KASKAZINI

Korea Kaskazini imesema familia nyingi nchini humo zimekumbwa na maradhi ya tumbo ambayo hayajatambuliwa chanzo chake.

Tatizo hilo limeongeza shinikizo katika mfumo wa afya wa nchi hiyo ambao tayari unatatizwa na UVIKO-19.

Serikali ya nchi hiyo ilitangaza kisa cha kwanza cha maambukizi ya UVIKO-19 mwezi uliopita, na kuanzisha mfumo mkali wa udhibiti uliosimamiwa moja kwa moja na kiongozi wake Kim Jong-Un.

Data zilizochapishwa na shirika la habari la nchi hiyo zinaonyesha kuwa tayari watu milioni 4.5 wamekwishaonyesha dalili za ugonjwa huo na 73 wamekwishapoteza maisha hadi jana.

Watu wengi miongoni mwa raia milioni 25 wa Korea Kaskazini hawajapata chanjo dhidi ya virusi vya corona. Baadhi ya ripoti zilisema kuwa maradhi ya tumbo yanaweza kuwa ni kipindupindu au homa ya matumbo inayoambatana na kuhara damu, na kwamba watu wasiopungua 1,600 wameathirika.



Picha iliyotolewa na shirika la habari la China Xinhua, ikionyesha manuari mpya yenye uwezo wa kutua ndege za kivita inayoitwa Fujian, baada ya kuzinduliwa juzi mjini Shanghai. **PICHA: Xinhua.**

# China yaunda manowari ya kubeba ndege vita

**BEIJING,** CHINA

China imezindua jana manowari yake ya tatu ya kubebea ndege za kivita, ikiwa ni ya kwanza kusanifiwa na kuundwa nchini humo.

Hatua hiyo inachukuliwa kama ishara kubwa ya kuimarika kijeshi kwa nchi hiyo ya bara la Asia.

Kufanikiwa kuundwa kwa chombo hicho kunakuja wakati mivutano ikizidi kushamiri kati ya China na Marekani kuhusiana na uhuru wa kisiwa cha Taiwan.

China inashikilia kuwa kisiwa hicho ni himaya yake, na kuwa itakichukuwa kwa nguvu ikiwa kitataka kujitangazia uhuru.

Manowari hiyo ijulikanayo kama Fujian ambayo ni ya kisasa zaidi kuliko nyingine za China, imezinduliwa kwenye kituo cha ujenzi wa meli mjini Beijing kukiwapo na shamra shamra za kipekee.

Itachukuwa miaka kadhaa kabla ya manowari hiyo kuingizwa katika operesheni, kwa sababu wizara ya ulinzi ya nchi hiyo haijatangaza tarehe ya kuanza kutumika.

**DW**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**TEGEMEZA AUCTION MART LIMITED**
**MBEZI BEACH TEL: 0719-187677**
**P.O. Box 77593 – DAR ES SALAAM.**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa mamlaka tuliyopewa na Mahakama Kuu kitengo cha Kazi, pamoja na mahakama ya mwanzo Sinza.

| AINA YA MALI | SEHEMU YA MNADA | MUDA | TAREHE YA MNADA | MADAI |
|---|---|---|---|---|
| GARI TOYOTA KLUGER T 637 DEC | MBEZI BEACH TANGI BOVU | SAA 4:30 ASUBUHI | 27/06/2022 SIKU YA JUMATATU | Kesi namba 230/2022 MDAI: BAHATI KAZIMIRI. MDAIWA: TREE-STAR-CO.LTD |
| NYUMBA | MPIJI MAGOE CCM DARAJANI | SAA 4:30 ASUBUHI | 29/06/2022 | Kesi namba 132 MDAI:SHEDDY JOHN SANGA MDAIWA:EMMY ABAS CHENGURA NA CLEMENCE SULEIMAN |

**MASHARTI YA MNADA**
- Mali inauzwa kama ilivyo unaweza kuja kukagua kabla ya tarehe ya mnada,
- Italipwa asilimia 25% siku ya mnada baada siku 14 itamaliziwa, usipomalizia uliyotoa awali haitarudishwa.
- Kwa mawasiliano zaidi **TEL: 0719-187677.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**FAIDHA SERECKY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0468-0012** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitria shule ya secondary ya **KIRIKI mwaka 2005,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Polisi taarifa HAN/RB/1436/2022**

### KUPOTEA KWA VYETI



**NEEMA ERNEST NGALI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato chane chenye index namba **S255-0073** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CAGLIERO GIRLS' SECONDARY SCHOOL** mwaka 1998 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0347/0683** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TAMBAZA HIGH SCHOOL mwaka 2001.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/CHU/RB/239442/2022**

### KUPOTEA KWA CHETI



**ABEL BASANDA MAYENGA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index no **S.4208/0063** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia shule ya Eloni Secondary School Mwaka 2017, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Taarifa ya Polisi, IGU/RB/2106/2021**

### KUPOTEA KWA CHETI



**BAHATI AUGUSTINO MBILINYI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1747-0090 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIBEREGE SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: KW/RB/2635/2020**

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Ndugu SELEMANI PAUL KULWA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya Toyota Premio lenye namba za usajili **T676 BVP** na injini namba **1ZZ0926416**. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/239215/2022**, kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige **simu namba 0758-638787.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MJINI DODOMA, Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 85/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU PLACID S. MAUFI wa DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA**
**MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA EVARIST S. MAUFI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imtolewa leo tarehe 16/06/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY SHABANI HUSSEIN ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya **TRELLA** yenye namba za usajili **T328BFH.** Chassis namba: **KWG17702** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/223062/2022.**

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY SHABAN HUSSEIN** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **GARI (HOZI)** yenye namba za usajili **T466CDM** Chassis namba**: 4467079** Injini namba **: 6156865** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/223065/2022.**

**KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD**
**COURT BROKER**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA **TAREHE 15 /07/2022 SAA NNE ASUBUHI** TUTAUZA MAGARI AINA YA TOYOTA **HILAX T263 BEB NA TOYOTA HARRIER T780 DPB** BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA UHUMA FINANCIAL SERVICES - DODOMA.
MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANO PIGA NO. 0688729841/ 0657222838.**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji.

# Kama ipo, ipo tu-**10**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani.

Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

*****************************************

Ilipita mwezi mmoja baada ya Bakari kuondoka. Siwatu alijiona kama anaishi kwenye kijiji kipya ambacho hakuwahi kuishi kabla.

Nafuu yake ni pale anapolala tu. Akiamka humuwaza Bakari. Hata mwenyewe alianza kujishangaa. Kumuwaza mtu ambaye hajawahi au kupata kuwa mpenzi wake. Hata hivyo alichojua yeye ni mazoea tu.

Pia ni kama wanakijiji walianza kumsuta. Alidhani kuwa baada ya kuondoka Bakari ambaye ndiye aliyesababisha atengwe, basi wanakijiji watamchangamkia kama zamani. Haikuwa hivyo.

Ni wachache tu waliokuwa wakiongea naye. Wengine walimbeza. Wapo waliomcheka.

"Hehee Hooiiii, ulidhani umepata bwana kutoka mbali, ukadharau watu wote kijijini, haya sasa huyoo kaenda kwao, kakuacha hapa hapa kupauka kama kipande cha muhogo." Kuna siku msichana mmoja alimwambia laivu, siyo kwa mafumbo wala nini.

Kwa kawaida alikuwa mpole. Hakutaka kugombana na mtu, hivyo alibaki kimya. Hata ile huruma kuwa mtoto yatima na kupata upendeleo maalum ilianza kupotea.

Hata hivyo hakupata hata siku moja kujutia kwa alichokifanya.

Usiku mmoja ambao ulikuwa na baridi kali na mvua za rasharasha. Ilipata saa saba au nane usiku. Alisikika kama mtu anavunja mlango.

Akahisi kama anaota. Lakini bado akasikia kama mtu anayejitahidi kuendelea kuvunja.




"Nani?" Akauliza kwa woga.

Hakujibiwa.

Akainuka kitandani kwa woga ili awashe koroboi. Akashuhudia kwenye mlango wa kuingilia chumbani kwake mtu mmoja aliyevaa mavazi marefu akiingia.

Akataka kupiga yowe, halikutoka.

Mkono wa mtu yule ambaye pamoja na kwamba hakuwasha taa aligundua kuwa ni mwanaume ulimshika.

Hakujua dhamira ni nini.

Mtu yule akamsukuma kitandani. kwa yale yaliyoendelea Siwatu aligundua dhamira ya mtu yule asiyefahamika ambaye hata sura aliificha, ni kumbaka.

"Mamaaa niache, Bakariii, nakufaaa." Akaita, lakini huyo anayemwita alikuwa ameshaondoka kiasi cha mwezi mmoja uliopita.

Sauti yake haikusikika mbali. Alitaka kufanya kila kitu ili kumzuia mbakaji huyo, akashindwa.

Kwa mbali alianza kusikia maumivu yasiyomithilika. Alitaka kupiga kelele tena, sauti haikutoka. Akajihisi kama mtu anayetumbukia kwenye shimo lenye kina kirefu lisilo na mwisho na baada ya hapo hakusikia kitu kingine tena.

*****************************

"Mwacheni apumzike, inatosha kumtazama, ondokeni hadi kesho tena." Ni sauti aliyoisikia kwa mbali kama ndoto.

Hakujijua yuko wapi. Kichwa chake kilikuwa kizito na maumivu makali. Alitaka kugeuka akashindwa.

"Umezinduka dada?" Ilikuwa ni sauti ya upole ya mtu ambaye hakumfahamu.

Kila sekunde ilivyozidi ndivyo akili ilivyokuwa inamrudia, lakini akizidi kushangaa mazingira aliyopo.

"Nipo wapi?" Akauliza.

"Pole sana dada upo kwenye zahanati ya kijiji cha Mkwega."

Siwatu aliitambua zahanati hiyo kuwa ipo kwenye kijiji cha tatu kutoka kijijini kwao Semwanza.

"Kwani nini kimetokea? Imekuwaje nimefika hapa?"

"Wewe bado mgonjwa, hujapona vizuri kwa hiyo si vizuri kukwambia yote, pumzika kwanza, kesho ndugu na jamaa zako watakuja. Kifupi ni kwamba umeletwa hapa jana asubuhi, ulikuwa hoi, na hakuna aliyetegemea kama ungepona. Inaonekana ni kama kuna mtu alikuvamia usiku..."

"Wewe ni nani?"

"Mimi ni nesi wa zamu ambaye nakuhudumia."

Alipomwambia hivyo, ndipo Siwatu aliporudisha kumbukumbu nyuma. Ni kweli akakumbuka alivamiwa na mtu ambaye alivunja mlango na kuingia ndani. Amevaa mavazi ambayo yalimfanya asionekana vema na alichomtendea ndicho kilichosababisha yeye kuletwa pale.

"Nashukuru sana nesi." Akasema kwa sauti ndogo ya mtu ambaye anapitia maumivu makali.

"Usijali, pumzika, usiongee kwa sababu ukiongea kuna maumivu unayapata, wewe lala mpaka kesho."

Kwa maana hiyo ni kwamba Siwatu aliingiliwa na mtu huyo usiku, hakuna aliyejua hilo hadi asubuhi ndipo walipompeleka hospitali na alikuwa amezirai, na akazinduka asubuhi saa nne wakati wanaokwenda kuangalia wagonjwa wao wameshaambiwa waondoke.

**Kwa mbali alianza kusikia maumivu yasiyomithilika. Alitaka kupiga kelele tena, sauti haikutoka. Akajihisi kama mtu anayetumbukia kwenye shimo lenye kina kirefu lisilo na mwisho na baada ya hapo hakusikia kitu kingine tena.**

Alilazwa kwenye zahanati hiyo kwa wiki nzima ndipo aliporuhusiwa kurudi nyumbani, lakini ikielezwa kuwa awe kwenye uangalizi maalum.

Sasa ilibidi kaka yake wa baba mkubwa na mdogo, Dibwela amchukue na kukaa naye kwake.

Kumbuka nyumba zote hizo mbili ni za Siwatu ambazo amezirithi kutoka kwa wazazi wake, lakini moja akampa kaka yake huyo.

Siwatu hakuwa na wazazi, na mume wala mpenzi kijijini hapo, hivyo isingekuwa rahisi kuwa chini ya uangalizi wowote kama madaktari walivyosema.

Ndiyo maana Dibwela alichukua jukumu hilo. Kibaya zaidi ni kwamba hata kaka yake hakuwa na mke, ila alikuwa na mpenzi tu aitwaye Mpaje, lakini hakai kwake.

"Pole wifi yangu."

"Ahsante Mpaje, hivi ilikuwaje hadi nikapelekwa zahanati mbona sielewi?" Siwatu aliuliza, siku mbili tu baada ya kutolewa kwenye zahanati.

"Shoga yako Mage alipita asubuhi kukujulia hali, akakuita lakini hukuitikia, lakini akashangaa kuona mlango uko wazi, kama haupo si ungekuwa umefungwa wakati unaishi peke yako? Akaamua kuingia, akapitiliza hadi chumbani ndiyo akakuta umelala, lakini siyo ulalaji wa kawaida, alipokusogelea karibu akagundua kuna tatizo, damu zilikuwa zinakutoka. Akatoka nje na kupiga kelele, watu tukaja kukuona, wakubwa wakaamua upelekwe zahanati ukatibiwe." Mpaje alimpa mkanda mzima wa kulichotokea wakati yeye akiwa amezirai.

"Basi mwenzangu." Siwatu alianza kumhadithia wifi yake, mpenzi wa kaka yake Dibwela.

"Usiku nimelala, nikasikia kama mtu anavunja mlango, kabla sijafanya kitu chochote naona mtu anaingia amejificha uso, nikajua nimekufa hapa, si ndiyo akanikaba shingoni akanitupia kitandani akanibaka." Akamalizia na sauti ya huzuni akaanza kulia.

"Basi Siwatu, basi wifi yangu, ni mitihani tu ya maisha, yatapita tu haya..."

"Kinachoniuma mimi Mpaje kwa nini anibake? Nimemkosea nini? Kwani mimi nimefanya baya gani hapa kijijini?"

"Hivi hadi anaondoka hukumjua ni nani?"

"Kwani alivyoondoka mimi nilikuwa mzima? Nilishazimia, angetaka hata kuniua angeniua. Na nilijaribu sana kutaka kumvua ile kofia yake kama ninja usoni na ile miguo yake, ili nihisi tu anaweza kuwa nani, lakini nilishindwa, alitumia nguvu nyingi kuhakikisha simfahamu. Kusema kweli wifi atakuwa ni mwanaume ambaye ananifahamu na mimi namfahamu..."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# JULIO ASEMA NAMUNGO FC HAIJAPOTEZA MWELEKEO

Na Adam Fungamwango

LICHA ya kufungwa mabao 2-1 na Polisi Tanzania, Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema bado hawajapoteza uelekeo kwenye mbio zao kuisaka nafasi ya tatu au ya nne kwenye Ligi Kuu ambazo zinaweza kuwafanya kupata nafasi ya kucheza michuano ya kimataifa.

**Akizungumza mara baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi na kupoteza nyumbani, Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, Julio amesema pamoja na kufungwa lakini bado wana mechi tatu mkononi na lolote linaweza kutokea.**

"Nilisema mpira wa sasa hivi unafungwa mahala popote, tumefanya makosa ya kizembe tumeadhibiwa, nikiri timu yao (Polisi Tanzania), ilikuwa vizuri zaidi kuliko ya kwetu.

Nadhani mapumziko tuliyoyapata yanaweza kuwa yameifanya timu isiwe kwenye mwendo wake wa kawaida, lakini tuna mechi tatu mbele, tunaweza bado kupata nafasi za juu, hatujapoteza mwelekeo na sisi tunaendelea kuitolea jicho nafasi ya tatu na ya nne. Lolote linaweza kutokea," alisema Julio.

Naye Kocha msaidizi wa Polisi, George Mketo alisema timu yao imeanza kurudi kwenye hali yake ya kawaida baada ya kutetereka kwenye mechi kadhaa kutokana na kuwa na majeruhi wengi.

"Timu yetu haikuwa na wachezaji wake wote, baadhi walikuwa majeruhi ndiyo maana tulipoteza sana hapa kati, sasa wamerejea ndiyo maana imekuwa nzuri, ambaye bado majeruhi ni Vitalis Mayanga tu," alisema Mketo, kiungo wa zamani wa Simba na Kagera Sugar.

Namungo iko kwenye nafasi ya tano ya msimamo ikiwa na pointi 37, huku Polisi Tanzania ikifuatia kwenye nafasi ya sita na pointi zake 36, zote zikibakisha mechi tatu tu kumaliza ligi.





Mfungaji bora wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya watu wenye ulemavu, Tembo Worriors, Khalifan Athuman Kihanga akitambulishwa Bungeni kwa ajili ya kupongezwa baada ya kufuzu kucheza kombe la Dunia.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# *Mabao 19 yamiminika raundi ya 27*

Na Adam Fungamwango

JUMLA ya mabao 19 yamefungwa kwenye mechi tisa za Ligi Kuu, raundi ya 27, huku timu za Coastal Union, Mbeya City na Ruvu Shooting zikipata vipigo vizito.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, uwanja pekee ambao haukuruhusu bao ni Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera ambako Jumanne iliyopita, Kagera Sugar ililazimishwa suluhu dhidi ya Biashara United.

Kwenye raundi hii ambapo zimebaki tatu tu ili kuhitimisha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, ni sare mbili tu zimepatikana kati ya mechi tisa zilizochezwa.

Ukiacha mechi ya suluhu kati ya Kagera Sugar dhidi ya Biashara United, nyingine ni KMC dhidi ya Prisons iliyochezwa Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, zikitoka sare ya bao 1-1.

Shughuli ilianza Jumatatu kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, mkoani Morogoro, Mtibwa ilipoichabanga Ruvu Shooting mabao 3-0, na Geita Gold ikiwa Uwanja wa Nyankumbu, Geita iliishindilia Dodoma Jiji mabao 2-0.

Mechi zingine ni Yanga kuisasambua Coastal Union mabao 3-0 Jumatano iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, siku hiyo hiyo, Azam FC ikaibamiza Mbeya Kwanza mabao 2-0, Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, juzi Alhamisi Simba ikairarua Mbeya City mabao 3-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku Polisi Tanzania ikiiadhiri Namungo mabao 2-0, Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

## Kocha Polisi awamwagia sifa wachezaji

Na Shufaa Lyimo

KOCHA msaidizi wa Klabu ya Polisi Tanzania, George Mketo amewapongeza wachezaji wake kwa kufanikiwa kupata pointi tatu kwenye mchezo wao dhidi ya Namungo FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha huyo alisema mchezo huo ulikuwa na ushindani mkubwa na wachezaji wake walipambana vizuri kupata ushindi huo ugenini.

"Ninawapongeza wachezaji wangu kwa kazi kubwa waliyoifanya kwenye uwanja wa Ilulu ingawa mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, lakini tumeondoka na pointi zote tatu," alisema Mketo.

Alisema baada ya mchezo huo timu hiyo ilianza safari jana asubuhi kurejea jijini Dar es Salaam kuendelea na mazoezi ya kujiwinda kukutana na timu ya Yanga katika mchezo ambao utapigwa Juni 22 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Alisema wanaiheshimu timu ya Yanga hivyo wanapaswa kuingia uwanjani wakifahamu wanakutana na Bingwa wa Ligi Kuu ya NBC msimu huu.

## Feitoto: Ubingwa nawapa mashabiki

Na Shufaa Lyimo

NYOTA wa Mabingwa wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' (pichani chini) amesema kuwa amefurahi kutwaa ubingwa msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili, mchezaji huyo alisema ubingwa huo ni zawadi kwa mashabiki wa Klabu hiyo pamoja na uongozi kiujumla.

Alisema mikakati yake ni kufanya vizuri katika michezo iliyobakia ikiwemo kubeba Kombe la Shirikisho (AF) na kumaliza ligi bila kupoteza.

"Malengo yangu ni kubeba Kombe la FA pamoja na kuvuna pointi tatu kwenye kila mchezo ambao tutaucheza, ninawashukuru mashabiki wangu kwa ushirikiano wanaonipa tangu nimefika kwenye Klabu hii," alisema Feisal.

Alisema atapambana kuhakikisha anazidi kuipa mafanikio Klabu yake hiyo na sasa akili na nguvu anazipeleka kwenye mchezo ujao wa Ligi Kuu, kabla ya kuelekea mkoani Arusha kuumana na Coastal Union kwenye mchezo wa Fainali wa Kombe la FA.

Aliahidi mashabiki wake kuwapa burudani katika mchezo huo ambao unasubiriwa na wadau mbali mbali wa soka.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JESUS AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumnasa mshambuliaji wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25. ***(Times)***

### POPE ATAKIWA

KLABU ya Newcastle United inamfuatilia mlinda mlango wa Burnley na England, Nick Pope mwenye umri wa miaka 30. ***(Mail)***

### BELLINGHAM AFUKUZIWA

LIVERPOOL wanamfukuzia kiungo wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham. ***(Mirror)***

### BOTMAN AWINDWA

KLABU ya Newcastle ina nafasi nzuri ya kumsajili mlinzi wa Lille na timu ya taifa ya Uholanzi wa chini ya umri wa miaka miaka 21, Sven Botman. ***(Football Insider)***

### CUCURELLA AWINDWA

KLABU ya Manchester City inajiandaa kupeleka ofa ya kumsajili mlinzi wa kushoto wa Brighton na Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 23. ***(Guardian)***

### LAVIA AGOMBEWA

KLABU za Leeds United na Southampton zinavutiwa na kiungo raia wa Ubelgiji, anayeichezea Manchester City, Romeo Lavia, 18. ***(Athletic)***

### BAZUNU SAFI

KLABU ya Southampton inatarajiwa kumtangaza kipa wa Jamhuri ya Ireland, Gavin Bazunu mwenye umri wa miaka 20 kutoka Manchester City kwa uhamisho unaofikia pauni milioni 15. ***(Telegraph)***

### PALHINHA AWANIWA

FULHAM na Wolves zinamtaka kiungo wa Sporting Lisbon na Ureno, Joao Palhinha, 26. ***(90min)***

### PEREZ NA HAALAND

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez amesema mshambuliaji mpya wa Manchester City, Erling Haaland, 21, asingeanza katika kikosi cha kwanza kama angehamia kwa klabu hiyo ya Hispania. ***(Mirror)***

### TARKOWSKI NA EVERTON

MLINZI James Tarkowski, 29, amekubali kujiunga na Everton mara mkataba wake wa sasa na Burnley utakapomalizima mwishoni mwa Juni. ***(Sky Sports)***

### DORTMUND NA BELLINGHAM

REAL Madrid wanatumaini kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, 18, licha ya ushindani kutoka kwa timu za Manchester United na Liverpool. ***(Metro)***

### FREDERICKS ATAKIWA

KLABU ya Bournemouth inakaribia kumsajili beki wa West Ham, Ryan Fredericks, lakini Fulham pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA AKUBALI KUSAINI MIAKA MINNE JUVENTUS

## ●●● Asema anataka kuzionesha klabu nyingine kuwa Man United walikosea kutompa mkataba...

**TURIN,** Italia

PAUL Pogba amekubali kujiunga na Juventus kwa mkataba wa miaka minne, kwa mujibu wa 90min.

**Kiungo huyo wa kati wa Ufaransa anatarajiwa kuondoka Manchester United kwa uhamisho huru kwa mara ya pili mwishoni mwa Juni, baada ya kushindwa kuafikiana kuhusu mkataba mpya pale Old Trafford.**

Kwa mujibu wa 90min Pogba ambaye ni mshindi wa kombe la Dunia na Ufaransa amekubali mkataba wa miaka minne kukaa pale kwenye Uwanja wa Allianz.

Licha ya kuwa na ofa kutoka Real Madrid na Paris Saint-Germain, Pogba ameamua kujiunga tena na Juve kutokana na mapenzi ya familia yake kwa jiji la Turin.

Uamuzi wa Pogba kujiunga na Juventus ni baada ya kuona timu hiyo ikijengwa upya na pia fursa ya kufanya tena kazi na kocha, Max Allegri.

Kiungo huyo bila shaka alifurahia misimu miwili bora ya klabu katika maisha yake ya soka chini ya Allegri kati ya mwaka 2014 na 2016, akishinda mara mbili ligi na kufika fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya.

Katika filamu yake mpya ya Amazon Prime 'Pogumentary', Pogba ametoa mwanga kuhusu mazungumzo yake ya mkataba na Man United kabla ya kuondoka.

"Mchakato wangu wa mawazo ni kuwaonesha Manchester kwamba, walifanya makosa kusubiri kunipa mkataba mpya na kuzionesha klabu nyingine kuwa walifanya makosa kwa kutonipa mkataba," alisema Pogba.

"Niliwaambia, 'Ikiwa wanataka nibaki, wasitoe ofa hiyo'. Nitawafanya waelewe kwamba, ikiwa kweli wanataka ubaki na wanataka kujenga mradi karibu na wewe, wakati huu wanapaswa kuchukua hatua tofauti na kuweka fedha mezani."


BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,006,4

MECHI KALI
KAGERA SUGAR
VERSUS
DODOMA FC
1 | 2.14
X | 2.76
2 | 3.70

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WAN-BISSAKA KUTUA CRYSTAL KWA MKOPO




**LONDON,** England

KLABU ya Crystal Palace imepewa nafasi kubwa ya kumsajili Aaron Wan-Bissaka kwa mkopo msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Uchezaji wa Wan-Bissaka pale Manchester United ulikwama msimu uliopita, huku majeraha na uchezaji mbaya ukimfanya achezee mechi 26 pekee kwenye mashindano yote.

Bahati yake ilishuka baada ya Ralf Rangnick kuchukua uongozi wa muda wa Mashetani Wekundu wakati wa msimu, huku Mjerumani huyo akipendekeza United kumuuza mchezaji huyo.

Na sasa Wan-Bissaka anaweza kuwa safarini msimu huu wa joto, ingawa kwa muda mfupi. United wako tayari kumwacha aondoke kwa mkopo msimu huu wa joto na klabu yake ya zamani ya Palace kwa sasa iko katika nafasi nzuri ya kupata huduma yake.

Kocha Jose Mourinho alikuwa na nia ya kumchukua Wan-Bissaka kule AS Roma, lakini timu hiyo ya Serie A badala yake imechagua kumfuata beki wa kulia wa Lille, Zeki Celik.

Palace sasa inajipanga kusajili mchezaji waliyemuuza United kwa karibu pauni milioni 50 mwaka 2019.

Wan-Bissaka anaonekana kuwa mchezaji wa hivi karibuni zaidi kuondoka United msimu huu wa joto huku Jesse Lingard, Nemanja Matic, Paul Pogba na Juan Mata wakiwa miongoni mwa wale ambao tayari wamefunguliwa mlango wa kutokea.




# FIFA yatangaza miji ya Kombe la Dunia la 2026

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la mpira wa miguu duniani, FIFA, limetangaza miji itakayoandaa kombe la Dunia la mwaka 2026 katika nchi za Marekani, Mexico na Canada.

Miji 16 imechaguliwa kutoka 22 katika mataifa hayo matatu ambayo kwa pamoja yanaandaa michuano hiyo.

Kwa Canada, hii ni mara ya kwanza kwa nchi hiyo kuandaa Kombe la Dunia la Wanaume, huku Marekani wakiwa wenyeji wa michuano hiyo mwaka 1994, na Mexico ilifanya hivyo mwaka 1970 na 1986.

Kombe la Dunia la 2026 litajumuisha ongezeko la timu na kuwa 48 kwa mara ya kwanza katika historia ya mashindano hayo na ni ya kwanza kuandaliwa katika mataifa matatu kwa pamoja.

Marekani itashi[...] Kombe lao la 11 la Du[...] baada ya pia kufaniki[...] mwaka huu nchini Qa[...] baada ya kukosa kush[...] ki Urusi mwaka 2018.

Mexico itashiriki k[...] mara ya 17 Kombe la D[...] nia na haijashindwa [...] fuzu tangu mwaka 19[...] huku Canada itakuwa [...] mara ya tatu baada [...] kufuzu kwa mashinda[...] hayo mwaka huu k[...] mara ya kwanza tan[...] mwaka 1986.

## HABARI MICHEZO


442,235/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/06/22 | 20:00 | Enppi Club vs Coca Cola | 3.47 | 2.92 | 2.28 |
| 02. 18/06/22 | 21:30 | Gimnasia Mendoza vs Deportivo Maipu | 2.28 | 2.78 | 3.68 |
| 03. 18/06/22 | 22:00 | Londrina PR vs Vasco da Gama | 3.26 | 2.86 | 2.42 |
| 04. 18/06/22 | 22:00 | Seattle Sounders vs Los Angeles FC | 2.30 | 3.53 | 2.97 |
| 05. 19/06/22 | 00:00 | Arsenal Sarandi vs Talleres | 2.60 | 3.10 | 2.90 |
| 06. 19/06/22 | 00:30 | Nautico PE vs Sport Recife | 2.73 | 2.97 | 2.73 |
| 07. 19/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Ceara CE | 2.65 | 3.10 | 2.75 |
| 08. 19/06/22 | 01:10 | Almirante Brown vs Deportivo Moron | 2.44 | 2.76 | 3.36 |
| 09. 19/06/22 | 01:45 | Sportivo Ameliano vs Nacional Asuncion | 2.77 | 3.12 | 2.57 |
| 10. 19/06/22 | 02:30 | Sarmiento vs Patronato Parana | 2.58 | 3.18 | 2.88 |
| 11. 19/06/22 | 03:00 | Chicago Fire vs DC United | 2.21 | 3.43 | 3.22 |
| 12. 19/06/22 | 13:30 | Suwon Samsung vs FC Seoul | 2.69 | 3.09 | 2.74 |
| 13. 19/06/22 | 17:00 | Guarani SP vs CSA AL | 2.42 | 2.97 | 3.12 |
| 14. 19/06/22 | 19:00 | Jerv vs Ham-Kam | 2.88 | 3.33 | 2.39 |
| 15. 19/06/22 | 21:00 | Aalesunds vs Valerenga | 2.46 | 3.39 | 2.74 |
| 16. 19/06/22 | 21:00 | Gimnasia Jujuy vs Temperley | 2.33 | 2.72 | 3.66 |
| 17. 19/06/22 | 22:00 | Tenerife vs Girona | 2.44 | 3.08 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 18/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2945 | Valmiera Fk/Bjss vs SK Super Nova | 1.09 | 7.82 | 19.56 |
| 15:00 | 1508 | Haka vs IFK Mariehamn | 1.67 | 3.64 | 4.42 |
| 15:00 | 1827 | Follo vs Halsen IF | 1.62 | 4.33 | 3.94 |
| 15:00 | 1842 | Vejgaard B vs Odder Igf | 2.18 | 3.68 | 2.70 |
| 15:00 | 2044 | Oppsal IF vs Sandviken | 1.85 | 4.43 | 3.00 |
| 15:00 | 2611 | Frederikssund vs Solroed FC | 1.29 | 5.71 | 6.69 |
| 15:00 | 2946 | BK Avarta vs BK Union | 1.25 | 6.07 | 7.25 |
| 15:00 | 5413 | Honka vs KuPS Kuopio | 2.69 | 2.98 | 2.54 |
| 15:00 | 5935 | TPS Turku vs KPV Kokkola | 1.54 | 3.84 | 5.31 |
| 15:15 | 1629 | Melaka vs Negeri Sembilan | 1.85 | 3.39 | 3.79 |
| 15:15 | 2062 | Sabah vs Pahang FA | 2.05 | 3.29 | 3.24 |
| 15:30 | 4849 | Dnepr Mogilev vs Neman Grodno | 5.89 | 3.73 | 1.51 |
| 16:00 | 1336 | Hawassa Kenema SC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.70 | 2.85 | 2.80 |
| 16:00 | 1562 | Geita Gold FC vs Biashara United | 2.32 | 2.65 | 3.44 |
| 16:00 | 1698 | KS Wisloka Debica vs Avia Swidnik | 4.13 | 4.13 | 1.62 |
| 16:00 | 2290 | Terengganu vs Kuala Lumpur | 1.99 | 3.29 | 3.39 |
| 16:00 | 3086 | Ellidi vs KFS | 1.65 | 4.14 | 3.94 |
| 16:00 | 3356 | Gicumbi vs Bugesera FC | 3.14 | 2.85 | 2.33 |
| 16:00 | 3765 | Japan U23 vs Australia U23 | 1.91 | 3.29 | 3.68 |
| 17:00 | 1077 | MP Mikkeli vs IF Gnistan | 2.27 | 3.39 | 2.75 |
| 17:00 | 1341 | EIF Ekenas vs Kerho 07 | 1.87 | 3.64 | 3.44 |
| 17:00 | 2242 | Sarpsborg vs Stromsgodset | 1.86 | 3.57 | 3.88 |
| 17:00 | 3751 | Dziugas vs Suduva | 6.11 | 4.14 | 1.44 |
| 17:00 | 4049 | Ilves Tampere vs Lahti | 1.82 | 3.54 | 3.74 |
| 17:00 | 4452 | KFG vs Sindri | 1.82 | 4.12 | 3.24 |
| 17:00 | 4465 | Fjardabyggd vs IR Reykjavik | 7.00 | 5.40 | 1.34 |
| 17:00 | 4755 | Fjolnir vs IF Vestri | 1.68 | 4.03 | 3.89 |
| 17:00 | 5122 | FF Jaro vs FC KTP | 2.21 | 3.30 | 2.91 |
| 17:00 | 5735 | Trans Narva vs Tallinna Kalev | 1.53 | 4.52 | 4.42 |
| 17:00 | 5926 | FK Vilnus Bfa vs FK Babrungas Plunge | 3.55 | 3.70 | 1.90 |
| 18:00 | 1845 | Rigas Futbola Skola vs FK Liepaja | 1.70 | 3.88 | 3.93 |
| 18:00 | 4645 | BATE Borisov vs Isloch | 1.30 | 4.73 | 8.29 |
| 18:00 | 5891 | Dinamo Samarqand vs Surkhon Termez | 2.38 | 2.76 | 3.15 |
| 18:15 | 5191 | Kagera Sugar vs Dodoma FC | 2.14 | 2.76 | 3.70 |
| 19:00 | 4560 | Kristiansund vs Bodo Glimt | 4.31 | 4.01 | 1.68 |
| 19:30 | 3383 | Paide Linnameeskond vs Kuressaare | 1.26 | 5.29 | 8.42 |
| 19:30 | 3586 | Magallanes vs Everton Vina del Mar | 2.55 | 3.40 | 2.55 |
| 20:00 | 1395 | Al Masry Club vs El Gouna | 2.14 | 3.11 | 3.51 |
| 20:00 | 1783 | PK-35 vs Japs | 1.81 | 3.59 | 3.73 |
| 20:00 | 3494 | Lamia vs FC Veria | 1.90 | 3.51 | 3.81 |
| 20:00 | 3927 | Dinamo Minsk vs Slutsk | 1.43 | 4.14 | 6.31 |
| 20:00 | 4189 | Enppi Club vs Coca Cola | 3.41 | 2.96 | 2.25 |
| 21:00 | 4627 | Weston FC vs FC Miami City Champions | 3.00 | 3.74 | 2.00 |
| 21:30 | 1248 | Longford Town vs Cork City | 3.72 | 3.87 | 1.74 |
| 21:30 | 4483 | Real Pilar vs Lujan | 1.90 | 3.39 | 3.58 |
| 21:45 | 4001 | Sligo Rovers vs Finn Harps | 1.86 | 3.19 | 4.03 |
| 22:00 | 4897 | Novorizontino SP vs Tombense MG | 2.02 | 2.94 | 3.77 |
| 22:00 | 5431 | Londrina PR vs Vasco da Gama | 3.14 | 2.79 | 2.36 |
| 22:30 | 2919 | El Ittihad Alexandria vs Misr Lel Makasa | 1.90 | 3.21 | 4.22 |
| 23:00 | 5539 | Hifk vs VPS Vaasa | 2.99 | 3.19 | 2.21 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# DROO SOKA LA UFUKWENI AFRIKA KUFANYIKA JUNI 24

**Na Adam Fungamwango**

DROO ya mechi za kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika Soka la Ufukweni inatarajiwa kufanyika Juni 24 mwaka huu.

**Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo (pichani) imesema kuwa jumla ya timu 14, ikiwemo timu ya taifa ya soka ya Tanzania kwa mchezo huo itakuwa inasubiri kwa hamu itapangwa na timu gani.**

Mbali na Tanzania timu zingine zinazosubiri droo hiyo, ni Cameroon, Comoro, Ivory Coast, Misri, Ghana, Libya, Madagascar, Malawi, Morocco, Nigeria, Senegal, Shelisheli, Tanzania na Uganda.

Taarifa imesema baada ya droo hiyo, timu hizo zitacheza hatua hiyo ya mtoano nyumbani na ugenini ili kupata washindi saba ambazo zitaungana na mwenyeji wa fainali hizo, Msumbiji na kuwa timu nane ambazo zitachuana kwenye fainali hizo kumsaka bingwa.

Imesema kwenye droo hiyo timu zimegawanywa kwa viwango na kijiografia, huku Tanzania ikiwa kwenye kundi la kiwango namba moja.

Taarifa ilisema timu za viwango namba moja kutoka kanda za Kusini mwa Afrika (COSAFA) na kanda ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) zitacheza na timu za kiwango namba mbili kutoka (COSAFA).

Timu za viwango namba moja kutoka kanda ya Afrika Kaskazini (UNAF) na Kanda ya Magharibi (WAFU A) na (WAFU B) zitacheza na timu za kiwango namba mbili za (UNAF) na (WAFU B).





Mmoja wa wanzilishi na wakurugenzi wa Taasisi ya The Pink Tie Foundation ambayo ina jishughulisha na masuala ya kumtetea mtoto wa kiume, Lillian Mwasha (katikati), akicheza muziki na watoto wa mitaani katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam juzi wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Seleman Sopu azungumzia usajili wake*

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Coastal Union, Abdul Seleman 'Sopu', ameweka wazi kuhusu usajili wake baada ya kupata ofa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya msimu ujao.

Nyota huyo amekuwa akihusishwa kurejea ndani ya klabu yake ya zamani ya Simba kwa kumuwekea mkataba mezani ili kwenda kuimarisha timu hiyo kwa msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sopu alisema bado ana mkataba na Coastal Union ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu na tayari kuna ofa ndani na nje ya nchi zimemfikia mezani.

Alisema kwa hapa Tanzania klabu kubwa zimefika mezani kwake, lakini hawezi kuzungumza suala hilo kwa sababu bado yuko katika mkataba na waajiriwa wake (Coastal Union).

"Ni kweli kuna ofa ziko mezani, lakini bado mazungumzo yanafanyika kwa sababu nina mkataba na Coastal Union ambao unamalizika msimu huu, baada ya hapo nitaweka wazi kuhusu muelekeo wangu wa msimu ujao," alisema Sopu.

Alisema kwa sasa anawapa nafasi uongozi wa timu yake hiyo ya sasa kama watakuwa tayari kumbakiza ndani ya timu hiyo na wakishindwa anafungua milango kwa klabu zinazomuhitaji.

# Michezo

Jumamosi Juni 18, 2022
Nipashe



**Pogba akubali miaka 4 Juve** UKURASA 21




Wachezaji wa Simba, Peter Banda na Pape Ousmane Sakho wakipongezana mara baada ya mchezo dhidi ya Mbeya City ambapo woa ndio walikuwa wafungaji wa mabao matatu wakati timu yao ikiibuka na ushindi wa 3-0, Alhamisi kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: SIMBA SC**

## Matola ataka Kibu Dennis avumiliwe

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola amewataka mashabiki wa klabu hiyo kumvumilia mchezaji wao, Kibu Dennis kutokana na kuonekana kushindwa mara kwa mara kumalizia kufunga mabao.

Akizungumza mara baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo dhidi ya Mbeya City, ikiondoka na ushindi wa mabao 3-0 juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Matola alisema ni kweli Kibu amekuwa akikosa baadhi ya nafasi za wazi za kufunga mabao, lakini anaamini kuwa anafundishika na baadaye atakuja kuwa mfungaji mzuri.

"Unajua siku zote sisi walimu tunaumia kama timu haitengenezi nafasi, lakini kama unatengeneza na mchezaji anakosa hilo linakuwa ni suala binafsi, unajua Kibu huwa tunakaa naye na kumweleza, pia tunamfanyisha mazoezi ya kufunga, nafikiri taratibu taratibu atabadilika, atafunga na kuwa mfungaji mzuri." Alisema Matola.

Kwenye mechi ya juzi, alikosa mabao mawili ya wazi ambayo kama angekuwa makini au kutulia, Simba ingeweza kutoka na ushindi mnene kwa mabao 5-0.

Mashabiki wa soka nchini, wa Simba na Taifa Stars wamekuwa wakimlaumu mchezaji huyo kutokana na kukosa nafasi za wazi.

Hata hivyo, mchezaji huyo amekuwa akipendwa sana wa makocha mbalimbali kutokana na uwezo wao mkubwa wa kukaa na mpira bila kunyang'anywa kirahisi, kujituma, kusaidia kukaba, na pamoja na kuwa msumbufu mno kwa mabeki, hivyo kuwarahisishia wenzake kazi, hali inayosababisha wawe wanapata nafasi kwenye vikosi vyote viwili, Simba na Taifa Stars.

# Mpole azitega Simba, Yanga

**Asema ni suala la muda tu itajulikana kama atacheza Msimbazi au Jangwani msimu ujao, huku Azam...**

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Geita Gold FC, George Mpole amesema ni suala la muda tu watu watajua ni wapi atacheza msimu ujao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, kati ya mtaa wa Msimbazi, Jangwani au kule Chamazi.

**Mpole anatajwa kuwa katika rada za kutakiwa na timu tatu kubwa hapa nchini kati ya Simba, Yanga na Azam FC ambapo inadawa kuwa ameshawekewa ofa mezani ya mkataba wa miaka miwili na mojawapo ya timu hizo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mpole amesema amepata ofa nyingi ikiwemo nje na hapa ndani, lakini hawezi kuweka wazi kwa sasa wapi msimu ujao atakakocheza.

Alisema bado ana mkataba na Geita Gold na mwishoni wa msimu huu atafikia tamati baada ya hapo kila kitu kitakuwa wazi ni timu gani atacheza msimu ujao.

"Kuna ofa zimekuja kwangu za hapa ndani na nyingine kutoka nje ya nchi, lakini suala la kujua wapi nitacheza msimu ujao bado tusubiri muda muafaka ukifika," alisema Mpole.

Aliongeza: "Ukifika muda muafaka kila kitu kitakuwa wazi wapi nitacheza kati ya timu zinazotajwa, au kubaki ndani ya Geita Gold."

Alisema kabla ya kuanza kufikiria ofa ambazo zimemfikia, kwanza anawapa kipaumbele Geita Gold ili aweze kuongeza mkataba mwingine na kuendelea kubaki ndani ya timu hiyo kabla ya kufikiria kupata changamoto nyingine.

Mpole kwa sasa anashika nafasi ya pili kwa wachezaji waliofunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu akiwa na mabao 15 nyuma ya nyota wa Yanga, Fiston Mayele mwenye mabao 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >